

**TOFAUTI ZA KIMOFONOLOJIA BAINA YA KIPEMBA CHA  
KASKAZINI NA CHA KUSINI**

**ASHA BAKAR SHARABIL**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA BAADHI YA  
MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UMAHIRI YA KISWAHILI  
(M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2017**

## **UTHIBITISHO**

Aliyeweka saina hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma kazi hii na anaidhinisha ikubaliwe kwa utahini na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania tasnifu yenye mada: *“Tofauti za Kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini”*, kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kutunukiwa Shahada ya M.A. Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

-----  
**Dkt. Hana Simpassa**

**(Msimamizi)**

Tarehe: -----

### **HATIMILIKI**

Tasnifu hii ya M.A. Kiswahili ni kazi inayolindwa kwa mujibu wa makubaliano ya kisheria. Kazi hii hairuhusiwi kutolewa kwa namna yoyote ile, iwe yote au sehemu isipokuwa kwa matumizi ya kitaaluma ya utafiti.

**IKIRARI**

Mimi **Asha Bakar Sharabil**, ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa wala haitowasilishwa katika chuo kikuu chochote kwa ajili ya shahada kama hii au nyingine yoyote.

.....  
Saini

.....  
Tarehe

**TABARUKU**

Kazi hii naitabaruku kwa wazazi wangu Bwana **Bakar Sharabil Ahmad** na Bi **Fatma Masoud** kwa malezi bora waliyonilea mtoto wao na kunipeleka shule kupata elimu. Kwa makusudio hayo, kazi hii naitabaruku maalumu kwa baba yangu mzazi marehemu Bakar Sharabil iwe kumbukumbu yake.

## SHUKURANI

Mwanzo kabisa, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyenijaalia uzima, afya njema na ustahamilivu katika kipindi chote cha masomo na utafiti huu. Kwa kweli hiki kilikuwa kipindi kizito ambacho misaada ya watu mbalimbali ya hali na mali ilihitajika. Nitakuwa mwizi wa fadhila, endapo nitashindwa kuwashukuru watu ambao wamechangia masomo yangu na ukamilishaji wa kazi hii. Hata hivyo, haitokuwa rahisi kuwataja wote kwa majina kwa sababu ni wengi, bali nitawataja wachache tu ili wawe ni wawakilishi wa wenzao.

Kwanza, namshukuru msimamizi wangu wa utafiti huu Dkt. Hana Simpassa kwa msaada wake mkubwa wakati wa usimamizi wa utafiti huu. Kwani yeye ndiye aliyeniongoza tokea nilipowasilisha wazo la utafiti, pendekezo na mchakato mzima wa utafiti. Kwa hakika bila ya usimamizi wake uliojaa busara na hekima kazi hii isingonekana kama ilivyo hii leo.

Pia, nitakuwa na deni lisilolipika bila kuwashukuru mwalimu Hamad Khamis Juma wa Chuo cha Kiislamu Pemba na mwalimu Bakar Kombo wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Tawi la Pemba kwa ushauri na maelekezo makubwa waliyonipatia wakati wa utafiti huu. Kwa hakika walimu hawa walinipa moyo pale nilipotamauka, kwa kunipa matumaini na kunielekeza njia za mafanikio.

Aidha, shukurani za pekee kwa Dkt. Lipembe, walimu na wanafunzi wenzangu wa Umahiri wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Tawi la Pemba kwa mashirikiano waliyonipa wakati wa masomo na utafiti huu. Bila kuwasahau watoa taarifa za data

ya uwandani kule Kaskazini na Kusini, Pemba. Ushirikiano wao umetoa mchango mkubwa katika kufanikisha kazi hii.

Mwisho, itakuwa ni muhali kwangu kusahau kutoa shukurani zangu za dhati kwa familia; mume wangu Bwana Kassim Ali Moh'd na watoto wetu Saad, Fatma, Saada, Ali, Moza, Ahmad na Nasir kwa upendo na uvumilivu mkubwa waliouonyesha wakati nikiwa nasoma na katika kipindi cha utafiti huu. Uvumilivu wao ulinipa matumaini na utulivu wa kuendelea na masomo yangu vizuri.

**IKISIRI**

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini ikiwa ni hatua mojawapo ya kuitafiti lahaja ya Kipemba . Data ya uwandani ya utafiti huu ilikusanywa kwa kutumia mbinu za dodoso, mahojiano na ushuhudiaji ambapo sampuli-kusudio na sampuli eneo zilitumika kwa ajili ya kuchagua watoa taarifa kwa vigezo vya umri na ukazi. Nadharia ya *Isimu Historia na Linganishi* imetumika katika kukusanya na kuchambua data ya utafiti huu. Nadharia hii imesaidia kubaini tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Katika kipengele cha kifonolojia ambacho kimechunguzwa, matokeo ya utafiti yanaonyesha kwamba kuna tofauti za kifonolojia zinazotokana na mpishano wa sauti, uchopekaji na udondoshaji wa sauti, ukaakaishaji na matumizi ya mpumuo. Kwa upande wa tofauti za kimofolojia, nazo zimejibainisha katika viambishi awali vya ngeli za nomino na uhamaji wa ngeli. Pia, kuna tofauti katika maumbo ya kitenzi katika viambishi vya nafsi, njeo, miishio ya baadhi ya vitenzi, utangamano wa irabu na kauli ya usababishi. Pamoja na kubainisha kuwa kuna tofauti za kifonolojia na kimofolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini, utafiti huu haukutoa hitimisho la moja kwa moja. Badala yake, tunapendekeza uchunguzi zaidi ufanyike kuchunguza asili na chimbuko la Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini.



## YALIYOMO

<b>UTHIBITISHO</b> .....	ii
<b>HATIMILIKI</b> .....	iii
<b>IKIRARI</b> .....	iv
<b>TABARUKU</b> .....	v
<b>SHUKURANI</b> .....	vi
<b>IKISIRI</b> .....	viii
<b>ORODHA YA MAJEDWALI</b> .....	xiii
<b>ORODHA YA VIFUPISHO NA FINYAZO</b> .....	xiv
<b>SURA YA KWANZA</b> .....	1
<b>1.0 UTANGULIZI WA JUMLA</b> .....	1
1.1 Utangulizi wa Sura .....	1
1.2 Jiografia ya Mahali pa Utafiti.....	1
1.2.1 Mkoa wa Kaskazini Pemba .....	2
1.2.2 Mkoa wa Kusini Pemba .....	3
1.3 Usuli wa Utafiti .....	3
1.4 Tatizo la Utafiti .....	5
1.5 Malengo ya Utafiti .....	6
1.5.1 Lengo Kuu.....	6
1.5.2 Malengo Mahususi .....	7
1.6 Maswali ya Utafiti .....	7
1.7 Umuhimu wa Utafiti.....	7
1.8 Mawanda ya Utafiti .....	8
1.9 Vikwazo vya Utafiti .....	8

1.10	Hitimisho la Sura.....	9
	<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>10</b>
<b>2.0</b>	<b>KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA .....</b>	<b>10</b>
2.1	Utangulizi wa Sura .....	10
2.2	Ufafanuzi kuhusu Dhana ya Lahaja .....	10
2.2.1	Fasili ya Dhana ya Fonolojia na Mofolojia .....	11
2.2.2	Utafiti wa Lahaja kwa Ujumla .....	12
2.2.3	Tafiti kuhusu Lahaja za Kiswahili .....	13
2.2.4	Tafiti kuhusu Lahaja ya Kipemba .....	14
2.3	Pengo la Utafiti.....	19
2.4	Kiunzi cha Nadharia.....	20
2.5	Hitimisho la Sura.....	21
	<b>SURA YA TATU .....</b>	<b>22</b>
<b>3.0</b>	<b>MBINU ZA UTAFITI.....</b>	<b>22</b>
3.1	Utangulizi .....	22
3.2	Mkabala wa Utafiti.....	22
3.3	Eneo la Utafiti .....	22
3.4	Walengwa wa Utafiti.....	23
3.5	Sampuli na Uteuzi wa Sampuli .....	23
3.6	Vyanzo na Aina ya Data.....	24
3.6.1	Data za Msingi .....	24
3.6.2	Data za Upili.....	25
3.7	Mbinu za Ukusanyaji wa Data .....	25
3.7.1	Hojaji.....	25

3.7.2	Mahojiano.....	26
3.7.3	Ushuhudiaji .....	26
3.8	Maadili ya Utafiti .....	27
3.9	Hitimisho la Sura.....	28
	<b>SURA YA NNE.....</b>	<b>29</b>
<b>4.0</b>	<b>UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA.....</b>	<b>29</b>
4.1	Utangulizi .....	29
4.2	Sauti za Kiswahili na Kipemba .....	29
4.2.1	Irabu .....	30
4.2.2	Konsonanti .....	30
4.2.3	Viyeyusho.....	30
4.3	Tofauti za Sauti .....	31
4.3.1	Tofauti za Mpishano wa Sauti.....	32
4.3.2	Mpishano wa Konsonanti.....	32
4.3.3	Mpishano wa Irabu.....	38
4.3.4	Mpishano wa Nusu-Irabu [w]:[y].....	38
4.3.5	Uchopekaji na Udondoshaji wa Sauti .....	39
4.3.6	Ukaakaishaji .....	43
4.3.7	Mchakato wa Mpumuo.....	44
4.4	Tofauti za Kimofolojia .....	44
4.4.1	Mofolojia ya Nomino .....	45
4.4.2	Mofolojia ya Kitenzi .....	48
4.4.3	Maumbo ya Njeo .....	50
4.4.4	Miishio ya Vitenzi .....	52

4.4.5	Tangamano Irabu.....	53
4.4.6	Kauli za Kitenzi.....	54
4.5	Hitimisho la Sura.....	55
<b>SURA YA TANO .....</b>		<b>56</b>
<b>5.0</b>	<b>MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....</b>	<b>56</b>
5.1	Utangulizi .....	56
5.2	Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti.....	56
5.2.1	Muhtasari wa Utafiti.....	57
5.2.2	Kujibu Maswali ya Utafiti.....	58
5.2.3	Mchango wa Utafiti.....	59
5.3	Hitimisho .....	60
5.4	Mapendekezo kwa ajili ya Tafiti Zaidi .....	61
<b>MAREJELEO .....</b>		<b>62</b>
<b>VIAMBATISHO .....</b>		<b>66</b>

**ORODHA YA MAJEDWALI**

Jedwali na. 4.1: Ngeli za Nomino .....	45
Jedwali na. 4.2: Viambishi vya Mtenda .....	48

**ORODHA YA VIFUPISHO NA FINYAZO**

BAKIZA	Baraza la Kiswahili la Zanzibar
Kisanifu	Kiswahili Sanifu
KKas	Kipemba cha Kaskazini
KKus	Kipemba cha Kusini
TATAKI	Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
Taz.	Tazama
§	Sehemu

## **SURA YA KWANZA**

### **1.0 UTANGULIZI WA JUMLA**

#### **1.1 Utangulizi wa Sura**

Sura hii inaeleza vipengele vinavyotoa taarifa za awali za utafiti kama vile jiografia ya mahali pa utafiti, usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wa vikwazo na mwisho ni muhtasari wa sura hii.

#### **1.2 Jiografia ya Mahali pa Utafiti**

Utafiti huu ulifanyika katika Kisiwa cha Pemba ambacho ni kisiwa dada cha Unguja katika visiwa vya Zanzibar. Kisiwa cha Pemba kiko katika Bahari ya Hindi umbali wa kilomita 40 kwenye upwa wa Afrika Mashariki. Kisiwa hiki kina ukubwa wa kilomita za mraba zipatazo 984 (Juma, 2011). Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 kisiwa hiki kilihesabiwa kuwa na wakazi wapatao 406,455 ambao hujulikana kama Wapemba. Kiutawala, kisiwa hiki kimegawika katika mikoa miwili ambayo ni mkoa wa Kaskazini na mkoa wa Kusini<sup>1</sup>.

Lugha kuu ya Wapemba ni Kiswahili kinachojulikana kama ‘lahaja ya Kipemba’. Wazungumzaji wa lahaja hii hutofautiana kifonolojia, kimsamiati na hata baadhi ya maumbo ya maneno kutoka eneo moja na jingine (Juma, 2011). Kwa mfano, Kipemba kinachozungumzwa Micheweni ni tofauti na kile kinachozunguzwa Kojani, hali kadhalika Kipemba kizungumzwacho Vitongoji ni tofauti na Kipemba cha

---

<sup>1</sup> Ripoti ya Sensa ya Watu na Makazi Tanzania 2012

Mwambe, Kangani na Chokocho. Katika kuchunguza tofauti za kimofonolojia utafiti huu ulifanyika katika mikoa ya Kaskazini na Kusini mwa kisiwa hiki.

### **1.2.1 Mkoa wa Kaskazini Pemba**

Mkoa wa Kaskazini una wilaya mbili ambazo ni wilaya ya Micheweni na wilaya ya Wete. Katika mkoa huu tulichagua vijiji vya Micheweni, Wingwi na Sebudawa ambavyo vimo katika wilaya ya Micheweni. Kijiografia, vijiji hivi vipo katika pembe ya Kaskazini mashariki ya Kisiwa cha Pemba. Katika utafiti huu vijiji hivi ndio vinavyowakilisha sampuli ya wazungumzaji wa Kipemba cha Kaskazini. Kwa mujibu wa utafiti wetu, watu wengi waishio Micheweni, Wingwi na Sebudawa, usemaji wao unaonekana kuwa umeathiriwa sana na lahaja ya Kipemba japokuwa wapo watu wachache ambao wanazungumza Kiswahili Sanifu. Utamkaji wa baadhi ya maneno ya watu wa Kaskazini unatofautina na utamkaji wa maneno ya watu wa Kusini kwa kiasi fulani.

Watu wengi waishio Micheweni, Wingwi na Sebudawa, kama sio wote, hawakuchanganya sana damu na wageni kutoka nje ya Afrika ambapo kiumbile na kisura wanaelekea kuwa Wabantu zaidi kuliko Waarabu (Mlacha, 1995). Watu hawa wana utamaduni mchanganyiko ambao unafanana na ule unaopatikana pwani ya Tanzania na Kenya na pia upo wa Kiarabu wenye athari kubwa ya dini ya kiislamu. Watu hao wametamakani katika eneo lenye ardhi tambarare iliyofunikwa na mawe. Kihali ya nchi, eneo hili ni nusu kame, ardhi yake haipokei kilimo vizuri. Kiuchumi, watu wa Micheweni hujishughulisha na uvuvi, kilimo kiasi, ufugaji na uchimbaji wa mawe ya kujengea nyumba.



### **1.2.2 Mkoa wa Kusini Pemba**

Mkoa wa Kusini Pemba una wilaya mbili; Wilaya ya Chakechake na Wilaya ya Mkoani. Katika mkoa huu tulichagua vijiji vya Mwambe, Jombwe na Shamiani ambavyo vyote vimo wilaya ya Mkoani. Kijiografia, vijiji hivi viko kusini mashariki ya kisiwa cha Pemba. Vijiji hivi vimepakana na bahari iliopo upande wa kusini mashariki ya kisiwa hiki. Usemaji wa watu waishio Mwambe, Jombwe na Shamiani umeathiriwa na lahaja ya Kipemba. Katika maeneo haya pia, wapo watu wanaotumia Kiswahili Sanifu katika maongezi yao ya kawaida. Hata hivyo, usemaji wa lahaja ya Kusini unatofautiana na ule wa Kaskazini.

Watu wa Kusini Pemba walio wengi ni Wabantu ambao hawakuchanganya sana damu na wageni kutoka Bara Arabu. Watu wa Mwambe, Jombwe na Shamiani wako katika eneo lenye ardhi tambarare iliyofunikwa na mawe. Kitabianchi, eneo hili ni nusu kame, ardhi yake haipokei kilimo vizuri. Kiuchumi, watu wa maeneo haya hujishughulisha na uvuvi, kilimo kiasi na ufugaji. Watu hawa wana utamaduni mchanganyiko, kwani kuna utamaduni unaopatikana sehemu za bara na pia kuna utamaduni wa kigeni, kama vile wa Kiarabu na Kiajemi. Kiimani, uislamu ndiyo dini inayotawala katika eneo hili lakini pia wapo waumini wachache wa dini nyingine (Khamis, 1984).

### **1.3 Usuli wa Utafiti**

Kiswahili ni lugha yenye chimbuko na inayozungumzwa sehemu za mwambao wa Afrika Mashariki (BAKIZA, 2010). Lugha hii inazungumzwa katika mitindo anuai kutegemea na eneo wanaloishi wazungumzaji. Mitindo hiyo mbalimbali ya

uzungumzaji kutokana na tofauti za watumiaji ndiyo huzaa lahaja. Lahaja ni tofauti za usemaji wa lugha zinazotokana na wazungumzaji wa lugha. Wazungumzaji hao wanaweza kutofautiana kifonolojia na pia katika baadhi ya msamiati usio wa msingi; maumbo na hata miundo. Tofauti hii ya uzungumzaji baina ya watumiaji wa lugha wa eneo moja na jingine husababisha kuachana kwa baadhi ya msamiati, fonolojia na miundo miongoni mwa wazungumzaji wa lugha moja. Tofauti hii inaweza kutokana na umbali wa kijiografia walionao wazungumzaji hao. Wakati mwingine, mtumiaji wa Kiswahili wa eneo fulani anaweza kudhaniwa hatumii Kiswahili kutokana na uzungumzaji wake kuathiriwa zaidi na uzungumzaji wa eneo analoishi na wakati mwingine anaweza kuongea kiasi cha kutoeleweka kabisa (Massamba, 2007).

Kwa mujibu wa King'ei (2010) lugha ya Kiswahili ina lahaja zisizopungua ishirini na moja. Miongoni mwa lahaja hizo ni pamoja na Kipemba kinachozungumzwa katika kisiwa cha Pemba, Kitumbatu kinachozungumzwa Kaskazini Unguja hadi katika kisiwa cha Tumbatu, Kimakunduchi (Kikae) kinachozungumzwa Kusini mwa kisiwa cha Unguja, Kimtang'ata kinachozungumzwa Tanga, Kijomvu kinachozungumzwa Kusini mwa Mombasa, Kimvita kinachozungumzwa Mombasa, Kipate kinachozungumzwa kisiwani Pate, Kibajuni kinachozungumzwa Kaskazini mwa Mombasa, Kiamu kinachozungumzwa Lamu, na kadhalika (King'ei, 2010; Habwe na Karanja, 2004).

Kuna tafiti mbalimbali ambazo zimewahi kushughulikia lahaja ya Kipemba, kama vile za Batibo (1982), Maganga (1991), Polomé (1967), Whiteley (1958), Khamis (1984). Hata hivyo, kazi hizi nyingi zimejikita katika kuangalia msamiati na

semantiki tu ya lahaja ya Kipemba. Tafiti hizo zimejikita zaidi katika maeneo mengine ya kiisimu na kuacha pengo katika kipengele cha fonolojia na mofolojia. Kwa mfano, Khamis (1984) aliangalia tofauti baina ya Kiswahili cha mjini na vijijini na kugundua kuwepo kwa tofauti za kimsamiati na kisintaksia.

Kuhusu kufanana au kutofautiana kwa Kiswahili cha Pemba watafiti kama Polomé (keshatajwa), Khamis (keshatajwa), Massamba (2006) na Juma (2011) wana maoni kuwa Kiswahili kinachozungumzwa Pemba kinatofautiana kutoka eneo moja na jingine. Kulingana na watafiti hao, kuna Kipemba kinachozungumzwa katika miji ya Wete, Chakechake, Mkoani na vijiji jirani vya miji hiyo, kwa kiasi kikubwa hufanana na Kiswahili Sanifu. Pia maeneo ya vijijini yanatofautiana kiuzungumzaji, kilafudhi na katika baadhi ya msamiati. Maeneo hayo ni kama vile Micheweni, Kojani, Kisiwapanza na Mwambe kwa kuyataja machache.

Aidha, wataalamu wengine (Batibo, 1982 na Maganga, 1991) wanalinganisha msamiati wa Kipemba na lahaja nyingine kama vile Kimakunduchi, Kipemba na Kiswahili Sanifu. Hata hivyo, hawakueleza kwa kina kuhusu tofauti za kimofonolojia zilizomo katika lahaja ya Kipemba. Kwa hiyo, utafiti huu umechunguza tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini kwani vipengele hivi havijaangaliwa kwa undani katika lahaja hii ya Kipemba.

#### **1.4 Tatizo la Utafiti**

Katika lahaja ya Kipemba kuna Kipemba kinachozungumzwa Kaskazini ambacho hutofautina na Kipemba kinachozungumzwa Kusini. Lugha inayozungumzwa katika

eneo kubwa, na hasa ikiwa baadhi ya maeneo yametengana na mengine kwa vipingamizi vya kijiografia kama vile: milima , mabonde, mito, maziwa, bahari na kadhalika au vizuizi vya kisiasa kama vile mipaka ya nchi, huwa na tabia ya kujiundia lahaja ambazo ni maalumu katika sehemu au eneo fulani. Lahaja hizi hujibainisha kuwa na tahajia tofauti kwa maneno ya lugha ileile, au kuwa na maneno tofauti kabisa na hata kuwa na sintaksia tofauti. Kaida hii ya lugha ndiyo iliyosababisha kuwepo kwa lahaja za Kiswahili (Mdee, 1998).

Kama tulivyokwishaeleza katika usuli, tafiti nyingi zilizokwisha fanywa kuhusu lahaja ya Kipemba, zinajikita zaidi katika kuchunguza msamiati na sintaksia. Hata hivyo, kwa mujibu wa uelewa wa mtafiti hakuna utafiti uliokwisha fanywa kwa ajili ya kuchunguza tofauti za kimofonolojia kati ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Jambo hili linaweka pengo la maarifa na kitaalamu katika lahaja hii. Kutokana na sababu hiyo, tunajiuliza maswali mengi yasiyo na majibu. Kwa mfano, tunajiuliza wazungumzaji wa Kipemba cha Kaskazini wanatofautiana vipi kifonolojia na wale wa Kusini, pia tofauti hizo za kifonolojia zinasababishwa na nini? Kwa hiyo, utafiti huu umechunguza tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini.

## **1.5 Malengo ya Utafiti**

Utafiti huu ulikuwa na lengo kuu na malengo mahususi yafuatayo:

### **1.5.1 Lengo Kuu**

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini.

### **1.5.2 Malengo Mahususi**

Utafiti huu ulibainisha na kulinganisha malengo mahususi yafuatayo:

- i) Kubainisha sauti za lugha ya Kiswahili Sanifu na sauti za lahaja ya Kipemba.
- ii) Kubainisha tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini.
- iii) Kutofautisha mofolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini.

### **1.6 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu umejibu maswali yafuatayo:

- i) Lugha ya Kiswahili Sanifu na lahaja ya Kipemba zina sauti zipi?
- ii) Kuna tofauti gani za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini?
- iii) Kuna tofauti gani za kimofolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini?

### **1.7 Umuhimu wa Utafiti**

Umuhimu wa utafiti huu unabainishwa na vipengele vikuu vifuatavyo kwanza, utafiti huu una umuhimu mkubwa sana katika taaluma ya lugha ya Kiswahili na lahaja zake kwa jumla. Utafiti huu ambao umechunguza tofauti za kimofonolojia katika lahaja ya Kipemba ni rejeo muhimu sana kwa wataalamu na wanafunzi wa isimu hususani katika mada hii ambayo ina marejeleo machache yaliyoandikwa kwa Kiswahili.

Pili, utafiti huu ni kichocheo cha watafiti wengine kufanya utafiti zaidi katika lahaja hii na lahaja nyingine. Aidha, utawasaidia watumiaji wa lugha ya Kiswahili katika

kuelewa tofauti za kifonolojia na kimofolojia zilizomo katika lahaja ya Kipemba, hususani Kipemba kinachozungumzwa Kaskazini (yaani maeneo ya Micheweni) na Kusini (yaani maeneo ya Mwambe).

Tatu, utafiti huu utakuza na kuongeza maarifa kuhusu fonolojia ya lahaja za Kiswahili na taaluma ya isimu kwa jumla. Hivyo basi, utatusaidia kulinganisha mofofonolojia ya lahaja mbalimbali za Kiswahili.

### **1.8 Mawanda ya Utafiti**

Utafiti huu umechunguza tofauti za kimofofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Kwa hiyo, haukujiielekeza katika kuchambua maswala ya msamiati na sintaksia kwa sababu kuchambua vipengele hivyo haikuwa lengo la utafiti huu. Pia, vipengele vya msamiati na sintaksia vimeshatafitiwa na watafiti wengine. Mawanda tumeyabana kutokana na kuzingatia ufinyu wa muda uliopangwa kufanya utafiti. Hata hivyo, hatuwezi kusema kuwa vipengele hivyo havikutajwa kabisa, bali vimeweza kubainishwa ili kutoa ufafanuzi katika utafiti huu pale ilipolazimu kufanya hivyo.

### **1.9 Vikwazo vya Utafiti**

Katika utafiti huu mtafiti alikutana na vikwazo kama vifuatavyo: Kwanza, katika ukusanyaji wa data, maneno ya Kipemba cha maeneo haya yalileta ugumu wa kuelewa kwa mtafiti kwa vile mtafiti haelewi vyema lahaja izungumzwayo katika maeneo haya. Mtafiti alitafuta watu wawili; mmoja Kaskazini na mmoja Kusini ambao wanaelewa vyema lahaja ya Kipemba kinachozungumzwa katika maeneo haya. Watu hawa walimsaidia mtafiti kwa kumfafanulia Kiswahili Sanifu kwa yale

maneno ambayo hakuyaelewa haraka. Aidha, mtafiti aliwatumia watu hawa kupata ufafanuzi zaidi wakati wa uchambuzi wa data ya uwandani.

Pili, katika ukusanyaji wa data lilijitokeza tatizo wakati wa mahojiano ambalo lilimfanya mtafiti aingize hisia zake na mitazamo binafsi kiasi cha data kukaribia kuathirika kiuhalisia. Hata hivyo, baada ya kuligundua hilo, mtafiti alitumia maswali elekezi ili kupata data inayokidhi kusudio la utafiti (taz. Kiambatisho A).

### **1.10 Hitimisho la Sura**

Katika sura hii tumeeleza vipengele vinavyotoa taarifa za awali za utafiti kama vile jiografia ya mahali pa utafiti, usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wa vikwazo. Sura inayofuata inahusu mapitio ya kazi tangulizi na kiunzi cha nadharia.

## **SURA YA PILI**

### **2.0 KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA**

#### **2.1 Utangulizi wa Sura**

Sura hii inabainisha na kuelezea mapitio ya kazi tangulizi. Katika kueleza mapitio ambayo yametumika katika utafiti huu tumeelezea tafiti za lahaja kwa ujumla na tafiti za lahaja za Kiswahili. Pia, sura hii inaelezea kiunzi cha nadharia iliyoongoza utafiti huu na mwisho ni hitimisho la sura.

#### **2.2 Ufafanuzi kuhusu Dhana ya Lahaja**

Kwa vile utafiti huu unahusu tofauti za kimofonolojia baina ya lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini, litakuwa jambo la maana sana iwapo tutaeleza japo kwa muhtasari dhana ya lahaja. Crystal (1985) anafasili maana ya lahaja kuwa ni mtindo wa lugha unaojibainisha kijiografia au kijamii, wenye msamiati na sarufi yake. Fasili kama hii imetolewa tena na TUKI (2004). Kwa mujibu wa wataalamu hawa, lahaja lazima ijibainishe kifonolojia, kimofolojia, kimsamiati na miundo ya sentensi.

Kwa ufupi, tunaweza kusema kuwa wasemaji wa lugha moja wanaweza kutofautiana kusemaji kulingana na maeneo walikosambaa. Huu ndio msingi wa lahaja ambao huakisi tofauti za lugha zinazojitokeza miongoni mwa wazungumzaji wa lugha moja wanapoachana kijiografia. Wazungumzaji hao wanaweza kutofautiana kifonolojia na pia katika baadhi ya msamiati usio wa msingi; na hata kimiundo. Katika lugha ya Kiswahili, tofauti hizo zinadhihirika katika lahaja zake. Hoja hii inazidi kushadidiwa



na Massamba (2004) pale anapoeleza kuwa lahaja ni lugha mojawapo kati ya lugha ambazo kimsingi huhesabiwa kuwa lugha moja isipokuwa zinatofautiana katika mambo madogo kama vile lafudhi au msamiati usio wa msingi.

Fasili hiyo ya lahaja inadhihirisha wazi kuwa tofauti kama hizo ziko katika maeneo mengi kunakozungumzwa Kiswahili. Tofauti za wazi kuhusu lahaja za Kiswahili katika maeneo mbalimbali zinajionyesha katika vipengele vya kifonolojia, kimsamiati, kimofolojia na kimiundo.

### **2.2.1 Fasili ya Dhana ya Fonolojia na Mofolojia**

Dhana ya fonolojia imefasiliwa na wataalamu mbalimbali. Kwa mujibu wa Lass (1984) fonolojia inahusika na utendaji, tabia na upangaji wa sauti kama viungo vya kiisimu. Naye Ladefoged (1975) anasema kuwa fonolojia inashughulikia kueleza mifumo na miundo ya sauti zinazopatikana katika lugha mahususi. Yule (1985) anasema kuwa fonolojia kimsingi ni maelezo ya mifumo na ruwaza za sauti za lugha. Kutokana na fasili hizo ni wazi kuwa fonolojia ni utanzu wa isimu unaochunguza jinsi sauti za lugha zinavyofanya kazi katika lugha mbalimbali.

Kabla hatujasema chochote kuhusu mofolojia ni muhimu kuelewa kuwa sauti za lugha ni tofauti na sauti nyingine ambazo pia hutolewa kupitia chemba ya kinywa au pua ya mwanadamu. Kwa mfano, sauti inayotoka wakati mtu anapopiga chafya, mluzi, mwayo au vigelegele (Massamba, 2004).

Dhana ya mofolojia inaelezwa kuwa ni neno linalotumiwa likimaanisha utanzu wa isimu unaoshughulikia muundo wa maneno. Hii ni taaluma ambayo hushughulikia

muundo wa ndani wa neno. Inaaminika kuwa maneno hujengwa kwa arki ziiwazo mofimu ambazo hutafitiwa katika mofolojia. Kwa hivyo, mofolojia huchunguza maswala kama vile aina za mofimu, namna mofimu zinavyojenga maneno na namna mofimu zinavyohusiana ili kuunda neno lenye maana. Kwa hivyo, kitovu cha uchunguzi wa kimofolojia ni neno, hivyo basi, ili kuelewa zaidi maana ya mofolojia na arki zake ni muhimu kufafanua maana ya neno. (Habwe na Karanja, 2004). Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa neno ni kipashio cha usemaji ambacho hujengwa na mofimu zilizopangika kisilabi na ambazo hutambuliwa na wasemaji wa lugha inayohusika kuwa kitu kimoja chenye maana mahususi. Kwa hiyo, neno ni kipashio kidogo lakini cha msingi katika lugha kwani ndicho kinachoweza msingi wa uchanganuzi wa kisintaksia.

### **2.2.2 Utafiti wa Lahaja kwa Ujumla**

Wataalamu wengi ulimwenguni wamejaribu kutafiti lahaja za lugha tofauti ili kulinganisha kufanana au kutofautiana kwa lahaja hizo katika vipengele mbalimbali vya kiisimu. Tafiti kuhusu lahaja za lugha nyingi duniani zilianza karne nyingi zilizopita. Katika sehemu hii tumeangalia tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusu lahaja.

Kortmann (2003) alifanya utafiti katika lahaja mbalimbali za lugha ya Kiingereza. Katika utafiti huo analinganisha maumbo ya maneno na sentensi katika lahaja za lugha hiyo. Katika utafiti wake aligundua kuwa lahaja ya Magharibi ya Uingereza ina sarufi ambayo ni tofauti na lahaja za visiwa vya Uingereza. Kwa mfano, wazungumzaji wa lahaja za Magharibi wanatofautiana kifonolojia na wazungumzaji

wa lahaja za visiwa vya Uingereza. Anaendelea kueleza kuwa hali hii si kwa lahaja ya Uingereza tu bali pia kwa lahaja za Scotland, Ireland ya Kaskazini na Jamuhuri ya Ireland. Aidha, katika lahaja hizo, kuna tofauti za kifonolojia na kimofolojia kwa baadhi ya maneno. Kupitia kazi hiyo, tunapata picha namna lahaja za lugha moja zinavyoweza kutofautiana kimofonolojia kwa baadhi ya maneno.

Prasad (2012) anatafiti lahaja za lugha ya Kichina ambapo anabaini kwamba Wachina wa eneo moja huzungumza tofauti na eneo jingine ambapo kuna mfanano wa kiwango kidogo sana. Kwa mfano, hali hiyo inabainika katika lahaja za Cantonese inayozungumzwa na watu wa Canton, Pekingese inayozungumzwa na watu wa Peking na Yunnanese inayozungumzwa na watu wa Yunani. Licha ya kwamba lahaja zote hizi zinapatikana katika jamiilugha moja na kuonesha mfanano lakini tofauti zipo kati yao. Kupitia kazi hii tunapata mwanga kuhusu tofauti za kimofonolojia za lahaja za lugha moja.

Kwa ujumla, tafiti hizi zinatupa picha ya namna wataalamu wa lugha na isimu ulimwenguni wanavyoshughulikia lahaja za lugha mbalimbali. Wataalamu hao huzichunguza lahaja kwa kuzilinganisha katika vipengele mbalimbali vya kiisimu ili kubaini kufanana au kutofautiana kwa lahaja hizo.

### **2.2.3 Tafiti kuhusu Lahaja za Kiswahili**

Wataalamu mbalimbali wamefanya tafiti na kuandika kuhusu lahaja za Kiswahili wakiwemo Sacleux (1909), Stigand (1915), Whiteley (1958), Polomé (1967), Chiraghdin na Mnyampala (1977), Khamis (1984), Maganga (1991), Kipacha (2003), na Massamba (2007) kwa kuwataja wachache.

Tafiti kuhusu lahaja ndogo za Kiswahili zimefanywa zaidi kwa lahaja za Kaskazini na Kusini. Massamba (2007) anatueleza kuwa lahaja zilizotafitiwa ni Kimtang'ata, ambayo ni lahaja ya Tanga na imetafitiwa na Whiteley (1957); Kivumba ambayo ni lahaja ya Vanga, mtafiti ni Lambert (1957); Kijomvu na Kingare ambazo ni lahaja ndogo za Kimvita zilizofanyiwa utafiti na Lambert (1958), Chichifundi lahaja ya Kusini Kenya, nayo ilifanyiwa utafiti na Lambert (1958), Lahaja za Pemba zilizotafitiwa na Whiteley (1958). Massamba anatueleza pia kuwa kuna tafiti chache zilizofanywa kuhusu lahaja nyingine kama vile Kimakunduchi, Kitumbatu na Kipemba.

#### **2.2.4 Tafiti kuhusu Lahaja ya Kipemba**

Lahaja ya Kipemba ina maandishi machache yaliyoandikwa na wataalamu kadhaa wakiwemo Sacleux (1909), Temu (1980), Stigand (1915), Whiteley (1956), Polomé (1967) kwa kuwataja baadhi yao.

Kazi ya kwanza kabisa kuhusu lahaja ni ya Sacleux (1909), ambaye alitafiti lahaja za Zanzibar. Kuhusu lahaja ya Kipemba, anaeleza kuwa Kipemba kina lahaja ndogo ndogo ambazo ni Kipemba cha Kusini, Kipemba cha Kivitongoji Mvumoni, Kipemba cha Chakechake na Kipemba cha Kimsuka ya Chaleni. Maelezo haya yanadhihirisha kuwako kwa tofauti ndogo ndogo ndani ya Kipemba tangu miaka hiyo katika maeneo kinakozungumzwa. Hata hivyo, kazi ya Sacleux haielezi chochote kuhusu tofauti za kimofonolojia katika lahaja ya Kipemba.

Stigand (1915) alitafiti kuhusu sarufi na mabadiliko ya lugha yatokanayo na tofauti za kilahaja katika lugha ya Kiswahili. Katika kazi hiyo, Stigand analinganisha baadhi

ya vipengele vya sarufi vya lahaja hizo. Miongoni mwa vipengele hivyo ni sauti, mofolojia na msamiati ambapo anabainisha mabadiliko ya kilahaja katika vipengele hivyo. Katika kufafanua lahaja ya Kipemba, Stigand anaeleza kuwa Kipemba ni lahaja ya kisiwa cha Pemba ambayo inafanana sana na lahaja ya zamani kwani ina maneno mengi ya wakazi wa kale wa kisiwa. Kazi hiyo ya Stigand inatupatia taarifa chache za kiisimujamii kuhusu lahaja ya Kipemba. Hata hivyo, Stigand hajabainisha tofauti za kifonolojia katika lahaja ya Kipemba; kazi ambayo imefanywa katika utafiti huu.

Johnston (1922) alieleza kuhusu lugha za Kibantu na lugha za Nusu-Bantu ambapo kuhusu Wapemba Johnston anaeleza kuwa inadaiwa kuwa Wareno walipofika Pemba walikiona kisiwa hicho kikiwa bado hakijakaliwa na wakawaleta wazigua na wasegeju kutoka bara. Zaidi, kazi ya Johnston inatupatia taarifa za kihistoria bila kubainisha tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini.

Ingrams (1924) ni mtaalamu mwingine aliyefanya utafiti katika Kiswahili cha Pemba. Kazi yake inalinganisha lahaja mbali mbali za Kiswahili zinazozungumzwa katika visiwa vya Unguja na Pemba. Kazi ya Ingrams, zaidi inalinganisha msamiati uliotumika katika lahaja za Kiswahili za visiwani kama vile Kipemba, Kihadimu na Kiunguja. Licha ya juhudi kubwa iliyofanywa na mtaalamu huyu, kazi yake haibainishi tofauti za kimofonolojia za lahaja hizo. Hata hivyo kazi yake kwa kiasi fulani ina mchango katika utafiti huu kwa sababu inatupatia taarifa fulani za kihistoria.

Whiteley (1958) aliandika kitabu kuhusu lahaja na mashairi ya Pemba. Kitabu hiki ni matokeo ya uchunguzi alioufanya mwaka 1957. Katika kitabu hicho, Whiteley anachambua sarufi za lahaja za maeneo mbalimbali ya Pemba. Vipengele vya sarufi anavyovibainisha ni kama vile msamiati, fonetiki, ngeli za nomino, aina za maneno na njeo. Katika kazi yake analinganisha vipengele hivyo na kubainisha namna vinavyotofautiana baina ya eneo moja na jingine. Anataja maeneo ambayo yanatofautiana kama vile, Micheweni – Wingwi (Pembe ya kaskazini mashariki ya kisiwa cha Pemba), kisiwa cha Kojani (mashariki), Matele [pengine Matale] – Kiuyu (kusini ya Kojani) na Kangani – Chokocho (kusini ya kisiwa cha Pemba). Pia, anaendelea kufafanua kuwa maeneo ya magharibi na katika miji ya Konde, Wete, Chakechake na Mkoani yameshaathiriwa na Kiswahili Sanifu. Kwa ujumla kazi ya Whiteley ina mchango katika utafiti wetu kwa sababu imeweza kuonesha maeneo ambayo kuna tofauti za kifonolojia katika lahaja ya Kipemba. Hata hivyo, kazi yake haijabainisha kwa kina tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini ambapo kazi ya kubainisha tofauti hizo imefanywa katika utafiti huu.

Polomé (1967) katika maelezo yake ya lahaja ya Kipemba, anaeleza kwamba maeneo ya Micheweni yana lahaja ndogo ambayo inatofautiana na maeneo mengine ya kisiwa hicho. Anazidi kueleza kuwa Kusini ya kisiwa cha Pemba hakuna ukaakaishaji wa kiambishi “ki” kabla ya nomino ambazo mizizi yake huanza na irabu. Pia, Polomé (1967) anaeleza maeneo yanayozungumzwa Kiswahili na watu wanaozungumza lugha hiyo, msambao wa lahaja za Kiswahili katika Afrika Mashariki, na maswala ya sarufi ya Kiswahili. Polomé pia, anaeleza tofauti za

kisarufi zinazojibainisha kwa baadhi ya lahaja. Hata hivyo, haelezi chochote kuhusu tofauti za kimofonolojia katika lahaja ya Kipemba.

Chiraghdin na Mnyampala (1977), wanaeleza kuwa Kipemba ni lahaja ambayo imechanganya maneno ya Kimtang'ata ambapo pia lahaja za Kivumba na Kimvita zina maneno machache ya Kipemba. Katika kazi yao wanatoa mfano wa msamiati wa Kipemba kama vile *ganja* 'siri', *gogwa* 'hasira', *uya* 'rudi' na kadhalika. Licha ya kutupatia taarifa za kiisimujamii na msamiati kuhusu lahaja ya Kipemba na kutuwekea mifano ya msamiati, kazi yao haijabainisha tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Kwa hakika, kazi ya kubainisha tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini imefanywa katika utafiti huu.

Batibo (1982) alifanya utafiti kulinganisha lahaja za Kiswahili cha Kusini, Kipemba kikiwa ni moja ya lahaja hizo. Utafiti huu ulilinganisha msamiati wa lahaja mbalimbali na kutoa mahitimisho kwa kusema kuwa lahaja zote hizo zinakaribiana. Kufuatana na matokeo haya lahaja zote zinaelewana kwa sababu kwa jumla hakuna matatizo katika kuwasiliana baina ya wazungumzaji. Kazi hii ya Batibo haioneshi tofauti za kimofonolojia katika lahaja za lugha; kazi ambayo imechunguzwa katika utafiti wetu.

Khamis (1984) alichunguza tofauti zilizopo baina ya Kipemba cha miji na vijijini. Utafiti wake ulichunguza tofauti hizo katika vipengele mbalimbali vya kiisimu. Katika kazi hiyo aligundua kuwa watu wote wa vijijini wanatofautiana kiuzungumzaji baina ya eneo moja na jingine. Kwa mfano, watu wa Micheweni

wanatofautiana na wale wa Kojani, watu wa Mwambe wanatofautiana na wale wa Matale na Chokocho pia. Hata hivyo, utafiti wake haukubainisha tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini; kazi ambayo imechunguzwa katika utafiti huu.

Maganga (1991) analinganisha lahaja za Kiswahili katika visiwa vya Zanzibar; Kiswahili sanifu, Kipemba, Kimakunduchi na Kitumbatu. Katika uchunguzi wake analinganisha mofonolojia ya lahaja hizi. Kupitia utafiti huo alibaini kuwa lahaja inayozungumzwa katika kisiwa cha Pemba haiko sawa kisiwa kizima, kuna lahaja tofauti kimaeneo hasa katika matumizi. Kazi yake haikubainisha ni lahaja zipi wala haikuchunguza tofauti za kimofonolojia baina ya lahaja hizo. Kwa hakika kazi ya Maganga imetoa mwanga katika utafiti wetu kwa kubainisha kuwa Kipemba kinatofautiana baina ya sehemu moja na nyingine. Kutokana na hoja hiyo tumehamasika kulinganisha mofonolojia ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini ili kubaini tofauti za kimofonolojia baina yao.

Kipacha (2004) alichunguza lahaja mbalimbali za Kiswahili katika mwambao wa Afrika ya Mashariki na visiwa vyake kama vile Chimiini, Kitikuu, Kipate, Kisiu, Kiamu, Kijomvu na Kingare. Lahaja nyingine ni Kivumba, Kimrima, Kipemba, Kiunguja, Kimakunduchi, Kitumbatu, Kimgao na Kingome. Katika kazi yake amebainisha tofauti zilizopo baina ya lahaja moja na nyingine akiwa amejikita zaidi katika kipengele cha msamiati na kwa uchache katika vipengele vya fonolojia na miundo. Hata hivyo, kazi ya Kipacha haionyeshi tofauti za kimofonolojia baina ya lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini.



Tafiti na kazi tangulizi zimemuwezesha mtafiti kugundua kuwa kuna pengo la kitaaluma katika kuelezea lahaja ya Kipemba. Kwa hiyo, panahitajika tafiti za kuchunguza lahaja ya Kipemba katika vipengele mbalimbali kikiwemo kipengele cha tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini ili kujaribu kuyaziba mapengo hayo.

### **2.3 Pengo la Utafiti**

Katika kusoma kazi tangulizi mbalimbali kwenye sehemu hii, mtafiti aligundua kwamba tofauti za kiisimu kama vile fonolojia na mofolojia zinaweza kujitokeza ndani ya lahaja moja. Kwa mfano, katika lahaja ya Kipemba kuna wataalamu kadhaa wanaoeleza kwamba Kipemba kinachozungumzwa katika sehemu moja ni tofauti na Kipemba kinachozungumzwa katika sehemu nyingine. Miongoni mwa wataalamu hao ni Whiteley (1958); Khamis, (1984), Maganga, (1991) na Massamba, (2006) kwa kuwataja wachache. Massamba (2006) anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili (lahaja) inayozungumzwa katika kisiwa cha Pemba hutofautiana kifonolojia, kimofolojia na kimsamiati kutoka eneo moja na jingine. Anaendelea kueleza kwamba ukienda Kojani kwa mfano, Kiswahili kinachozungumwa katika kisiwa hicho kinatofautiana na kile kinachungumzwa Micheweni na maeneo mengine ya Pemba.

Hapo, mtafiti aligundua kwamba utafiti wa kulinganisha Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini hususani katika kipengele cha mofonolojia haujafanyika. Jambo hili linaweka pengo la kiutafiti ambalo linahitaji kushughulikiwa. Utafiti huu umetofautisha mofonolojia ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini.

## 2.4 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu umetumia *Nadharia ya Isimu Historia na Linganishi*. Nadharia hii iliasisiwa na William Jones mwaka 1786 wakati alipolinganisha lugha za Kisankriti, Kigiriki na Kilatini ili kubaini uhusiano wa kimnasaba wa lugha hizo. Nadharia hii hufanya kazi katika viwango viwili; kwanza, huzilinganisha lugha mbili au zaidi kuonesha jinsi zinavyofanana au zinavyotofautiana; aghalabu kwa kuzingatia zilivyo katika wakati wa hivi sasa. Pili, huchunguza maendeleo ya lugha katika kipindi fulani cha historia ambapo kipindi hicho kinaweza kuwa cha nyuma sana, cha kati au cha hivi karibuni. Katika kuzilinganisha lugha mbili au zaidi ili kuona uhusiano wake wanaisimu hutumia mbinu inayojulikana kama mbinu linganishi. Anttila (1972) aeleza kuwa mbinu linganishi ni mbinu inayotumiwa kuchambua lugha zaidi ya moja ambazo zina asili moja ili kuonesha uhusiano wake wa kihistoria. Kwa kutumia mbinu hii lugha huchunguzwa katika vipengele vya kiisimu kama vile, msamiati wa msingi, fonolojia, mofolojia, sintaksia, ngeli za nomino, na kadhalika.

Katika utafiti huu tumeitumia mbinu linganishi ambayo imetusaidia kulinganisha mofofonolojia ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Kupitia mbinu hii tumeweza kuchunguza maneno na kuona kuwa kuna maneno yanatofautiana katika baadhi ya sauti kwenye maumbo yake. Maneno haya yanayotofautiana kimaumbo kwa baadhi ya sauti lakini yakiwa na ukubalifu wa sauti hujulikana kama maneno mnasaba (Massamba, 2002).

Kwa hivyo, katika utafiti huu tumetumia mbinu linganishi kutofautisha mofofonolojia ya maumbo ya maneno ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini.

Kwa ujumla, nadharia ya *Isimu Historia na Linganishi* na *Mbinu Linganishi* zimetusaidia kukusanya na kuchambua data ya utafiti huu na kupata matokeo ambayo tumeyabainisha katika tasnifu hii.

## **2.5 Hitimisho la Sura**

Katika sura hii tumebainisha na kujadili mapitio ya kazi tangulizi. Katika kujadili mapitio ya kazi tangulizi ambazo zimetumika katika utafiti huu tumeelezea tafiti za lahaja kwa ujumla na tafiti za lahaja za Kiswahili. Pia, tumebainisha kiunzi cha nadharia iliyotumika kuongoza utafiti na kubainisha pengo la utafiti. Sura inayofuata inaelezea mbinu za utafiti zilizotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data.

## **SURA YA TATU**

### **3.0 MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Sura hii inajadili mbinu za utafiti ambazo mtafiti alizitumia katika mchakato mzima wa utafiti huu. Vipengele ambavyo vimeshughulikiwa ni mkabala wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, sampuli. Pia tumeelezea mbinu za ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa data, maadili ya utafiti na hitimisho la sura hii.

#### **3.2 Mkabala wa Utafiti**

Utafiti huu ni wa uchunguzi makini ambao ulitumia muundo wa kimaelezo kukusanya na kuchanganua data. Utafiti wa kimaelezo kwa mujibu wa Cohen na wenzake (2000) hupanga na kutoa sababu na kuzieleza data kama zilivyoelezwa na walengwa wa utafiti. Data zilipangwa kutokana na maudhui au makundi yanayolingana. Muundo huu ni muhimu kwani umemsaidia mtafiti kufafanua dhana zilizofungwa, na pia maelezo yaliyotolewa na washiriki yalipatiwa ufafanuzi wa kina.

#### **3.3 Eneo la Utafiti**

Utafiti huu ulifanyika katika kisiwa cha Pemba katika mikoa ya Kaskazini na Kusini. Mkoa wa Kaskazini ulihusisha maeneo ya Micheweni, Wingwi na Sebudawa. Pia, mkoa wa Kusini ulihusisha maeneo ya Mwambe, Jombwe na Shamiani. Mtafiti aliteua maeneo hayo kwa sababu ni maeneo ambayo hadi hii leo wakazi wake walio wengi wanazungumza zaidi lahaja zao kuliko Kiswahili Sanifu. Pia, maeneo haya

yalitupatia uwakilishi mzuri wa tofauti za kimofonolojia tulizozichunguza kwa sababu maeneo hayo yameachana kijiografia.

### **3.4 Walengwa wa Utafiti**

Walengwa wa utafiti ni watu wote au hata mtu mmoja, kundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake (Kothari, 2009). Kwa mujibu wa Adam na Kamuzora (2007) usampulishaji ni mbinu, mchakato au kitendo cha kuwatafuta walengwa wa utafiti. Kwa hiyo walengwa wa utafiti huu ni wakazi wote wa Kaskazini na Kusini Pemba.

Katika utafiti huu walengwa wa utafiti walikuwa ni wazungumzaji wazawa wa lahaja ya Kipemba. Hivyo basi, walengwa walikuwa makundi mawili ambapo kundi la kwanza walikuwa watu wazima wa makamo wenye umri kuanzia miaka 50 na kuendelea ambao walidodoswa na kutoa taarifa. Kundi la pili ni wajuzi wa lugha ambapo walimu wa shule wanaofundisha masomo ya lugha ambao pia ni wazawa wa lahaja walishiriki katika majadiliano na kujaza hojaji. Tulichagua walimu wa shule ili kusaidia mjadala wa uchambuzi wa sauti za Kipemba na sababu zinazochangia tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini.

### **3.5 Sampuli na Uteuzi wa Sampuli**

Sampuli ni aina au mfano wa kitu (TUKI, 2004). Kuhusu sampuli ya watafitiwa tunaweza kusema kuwa ni kitu kimoja kati ya vingi kilichochaguliwa kuwakilisha vitu vinavyofanyiwa uchunguzi ili kupata taarifa za uchunguzi huo. Katika utafiti huu tulitumia mbinu ya usampulishaji kusudio katika ukusanyaji wa data. Hii ni aina

ya usampulishaji ambayo mtafiti anachagua sampuli kulingana na malengo maalumu. Tutilumia usampulishaji kusudio kwa sababu tulichagua wahojiwa kwa vigezo vya umri na ukazi.

Kwa mujibu wa Kothari (2009), uzuri wa utafiti ni kwa mtafiti kuchagua watoa taarifa wanaofaa kwa utafiti wake. Hivyo sampuli kusudio na sampuli eneo ilimsaidia mtafiti kupata watoa taarifa anaowataka. Utafiti huu ulihusisha watafitiwa 40 ambapo watafitiwa 20 walitoka mkoa wa Kaskazini na 20 mkoa wa Kusini, Pemba ambapo sampuli ilizingatia kigezo cha umri na ukazi. Katika kuchagua watoa taarifa hao, tulijielekeza zaidi kuchagua watu wazima zaidi ya miaka 50 kwa sababu watu hawa hawajapata athari kubwa ya Kiswahili Sanifu katika maeneo hayo.

### **3.6 Vyanzo na Aina ya Data**

Data za utafiti zilikusanywa kwa njia ya maelezo. Kuna vyanzo vikuu viwili vya data ambavyo vilitumika katika ukusanyaji wa data za utafiti ambavyo ni maktabani na uwandani. Katika utafiti huu tulikusanya data za msingi na data za upili. Hivi ndivyo vyanzo vikuu vya data ambazo zilikusanywa na kutumika katika utafiti huu.

#### **3.6.1 Data za Msingi**

Data za msingi ni data ambazo zimekusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti kutoka uwandani. Kothari (2009) anaeleza kuwa hizi ni data zinazokusanywa kutoka kwa wahojiwa ambazo ndio data halisi. Kwa sababu data hizi zinajumuisha hisia, imani, thamani na mitazamo ya watoa taarifa kwa undani. Data hizi mtafiti huzipata uso kwa uso kutoka kwa watoa taarifa wake wa uwandani. Data za msingi zimekusanywa kwa njia ya hojaji, mahojiano na ushuhudiaji.

### **3.6.2 Data za Upili**

Data za upili hukusanywa kutoka katika vyanzo kama vile vitabu, majarida, magazeti na machapisho mengine yanayopatikana maktabani, mitandaoni na kadhalika (Adams na wenzake). Mtafiti hukitumia chanzo hiki cha data katika kupata data ya awali ambazo huzitumia katika uandaaji wa pendekezo la utafiti wake. Data za aina hii zinaweza kuwa zimechapishwa au hazikuchapishwa lakini zinapatikana maktabani au hata mitandaoni (Kothari, keshatajwa).

## **3.7 Mbinu za Ukusanyaji wa Data**

Kukusanya data ni zoezi la awali katika utafiti. Kothari (2009) anaifafanua dhana ya ukusanyaji data kama zoezi la awali katika utafiti ambalo humwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusanya ili kumfikisha kwenye malengo yake ya utafiti. Anasisitiza kuwa hatua ya uwasilishaji na uchanganuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua hii ya ukusanyaji data. Katika utafiti huu mtafiti alitumia njia mbalimbali katika kukusanya data, njia hizo ni hojaji, mahojiano na ushuhudiaji.

### **3.7.1 Hojaji**

Hojaji ni mbinu ya utafiti ambayo mtafiti huandaa maswali yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani (Kothari, 2009). Maswali haya yanaweza kuhitaji majibu mafupi au marefu kutegemea taarifa inayohitajika kutoka kwa mtu anaedodoswa.

Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti kukusanya data ambazo alizipata kutoka kwa wamilisi wa lugha katika maeneo husika. Katika utafiti huu mbinu hii ilimsaidia mtafiti kukusanya data za tofauti za kimofonolojia za Kipemba cha Kaskazini na cha

Kusini katika vijiji teule. Kwa kutumia mbinu hii mtafiti aliwahoji watu wazima katika vijiji vilivyoteuliwa. Mbinu ya hojaji ilitumika ili kupata data kuhusu tofauti za kimofonolojia za lengo mahususi la pili na la tatu. Jumla ya watu wazima 20 walisailiwa ambapo 10 kutoka Kaskazini na 10 walitoka Kusini.

### **3.7.2 Mahojiano**

Mahojiano ni mbinu ambayo taarifa hukusanywa kwa njia ya kuuliza maswali ana kwa ana au simu. Kwa mujibu wa Kothari (2009) mbinu ya mahojiano ni mbinu ya ukusanyaji data ambayo huhusisha kuuliza maswali kwa njia ya mdomo na kupata majibu kwa njia hiyo hiyo. Maswali hayo yanaweza kuhitaji majibu mafupi au marefu kutegemea na taarifa inayohitajika na mtu anaepewa hojaji hizo. Mbinu hii ilitumika kupata usuli wa wakazi wa maeneo ya utafiti, kama vile asili yao, kazi zao na lugha zao. Pia mbinu hii ilisaidia kupata data za tofauti za mofonolojia ya lahaja ya Kipemba ambayo ilitumika kufikia lengo mahususi la pili na la tatu.

Faida ya njia hii ni pamoja na kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa watafitiwa wasiojua kusoma au kuandika. Pia huokoa muda kwani mtafiti anaweza kuhojiana na watafitiwa wengi kwa wakati mmoja kwa kutumia majadiliano ya pamoja. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kuthibitisha taarifa zilizopatikana kwa njia nyingine kama hojaji.

### **3.7.3 Ushuhudiaji**

Ushuhudiaji ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambayo mtafiti hukusanya data katika hali yake ya asili. Kwa mujibu wa Kothari (2004) ushuhudiaji ni mbinu ambayo taarifa hukusanywa na mtafiti mwenyewe kwa kushuhudia tabia za watafitiwa wake



bila ya kuwauliza maswali yoyote. Nunan (1992) na Adewole (1984) wanadai kuwa ili kugundua tabia fulani mtafiti hana budi kuichunguza katika mazingira ya utokeaji wake. Katika mbinu hii taarifa hupatikana kwa njia ya kushuhudia, ambapo mtafiti hutumia uwezo wa kuona, kusikia, kuonja, kunusa na kugusa vitu.

Katika utafiti huu mtafiti ameshuhudia mwenyewe jinsi mazungumzo yanavyofanyika katika maeneo ya matumizi ya lugha asilia kama vile nyumbani, mitaani na sokoni. Mazungumzo ya watafitiwa yalimsaidia mtafiti kubaini tofauti za kimofonolojia zinazojitokeza. Data iliyokusanywa kwa mbinu hii ilisaidia kuthibitisha data zilizokusanywa kwa mbinu za hojaji na usaili.

Utafiti huu ulitumia mbinu mchanganyiko za ukusanyaji wa data kwani katika mbinu za utafiti wa kisayansi jamii, inapendekezwa kutumia mbinu zaidi ya moja katika ukusanyaji wa data za kuchunguza tabia changamani za binadamu (Cohen na wenzake, 2000). Kwa vile kila mbinu ina udhaifu katika kupata taarifa zinazohitajika, utumiaji wa mbinu zaidi ya moja unamwezesha mtafiti kuthibitisha, kuhakiki na kurekebisha data alizozikusanya. Kwa sababu hiyo, data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usaili, hojaji na ushuhudiaji.

### **3.8 Maadili ya Utafiti**

Katika kufanikisha utafiti huu mtafiti lazima aeleze maadili kwa watafitiwa ili kutoa taarifa za kweli bila ya woga. Kwa mujibu wa Sture (2010) mkabala wa maadili ni mojawapo ya maswala muhimu ambayo mtafiti anapaswa kuyazingatia kwa uzito wake wakati akifikiria, akipanga, kutekeleza na hata baada ya kukamilisha utafiti

wake. Pia Adam na wenzake (2008) wametaja maadili ya utafiti ni haki ya kuwa na usiri yaani mtafiti hatatoa siri za mtafitiwa. Anafafanua kuwa haki ya mtafitiwa ni kuhakikishiwa usalama wake, haki ya kujua madhumuni, haki ya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu swali atakalopenda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti. Hivyo katika utafiti huu mtafiti alitumia kibali alichopewa na chuo na kuomba vibali kutoka serikali za mikoa ili kujitambulisha na kuwahakikishia usalama watoa taarifa wake.

### **3.9 Hitimisho la Sura**

Katika sura hii tumeeleza mbinu za utafiti ambazo mtafiti alizitumia katika mchakato mzima wa utafiti huu. Vipengele ambavyo vimebainishwa ni muundo wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, sampuli na mbinu za ukusanyaji wa data. Pia tumeelezea mbinu za uchambuzi na uwasilishaji wa data, maadili ya utafiti na muhtasari wa sura hii. Sura inayofuata inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data.

## **SURA YA NNE**

### **4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA**

#### **4.1 Utangulizi**

Sura hii inachambua na kuwasilisha data zinazohusu tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini zilizokusanywa kutoka uwandani. Matokeo ya utafiti yamewasilishwa katika sehemu hii ambapo katika uwasilishaji wa data hiyo, tumeanza kwa kubainisha sauti za lugha ya Kiswahili na sauti za lahaja ya Kipemba. Pia, tumebainisha tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini na kumalizia kwa kubainisha tofauti za kimofolojia baina ya lahaja ya Kipemba kinachozungumzwa katika maeneo hayo.

Katika uchambuzi huu tunaukilia kuchambua malengo mahususi ya utafiti wetu ambayo yamebainishwa katika § 1.4.2. Uchambuzi wa malengo mahususi hayo ni kama unavyoonekana katika sehemu zitakazofuata hapa chini.

#### **4.2 Sauti za Kiswahili na Kipemba**

Katika sehemu hii tumechambua data kuhusu lengo mahususi la kwanza la utafiti huu ambalo lilihusu kubainisha sauti za lugha ya Kiswahili Sanifu na za lahaja ya Kipemba. Kabla hatujabainisha na kujadili tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini, tumechunguza mifumo ya sauti za Kiswahili Sanifu. Kwa sababu, lugha zinatofautiana katika idadi ya sauti zitumikazo katika mfumo lugha. Hapa, tumechunguza sauti za Kiswahili Sanifu na sauti za lahaja ya Kipemba ili kulinganisha na kulinganua mifumo hiyo ya sauti. Katika uchambuzi

wetu tumezigawa sauti za lugha katika makundi matatu; ambayo ni irabu, konsonanti na viyeyusho.

#### **4.2.1 Irabu**

Irabu ni aina ya vitamkwa ambavyo hutolewa pasi na kuwepo kizuizi chochote katika mkondohewa utokao mapafuni ukipitia katika chemba ya kinywa na chemba ya pua (Massamba na wenzake, 2004). Utafiti wetu unabainisha kuwa mifumo ya irabu baina ya Kiswahili Sanifu na lahaja ya Kipemba iko sawa. Hivyo, kuna irabu tano; ambazo ni a, e, i, o na u. Katika irabu hizo, i na u ni irabu za *juu*; e na o ni za *kati*; na a ni ya *chini*. Pia, irabu i na e ni za mbele na hutamkwa kwa mtandazo wa mdomo, irabu a si ya mbele wala nyuma bali hutamkwa kwa midomo mtandazo. Irabu o na u ni za nyuma na hutamkwa kwa midomo iliyoviringwa.

#### **4.2.2 Konsonanti**

Konsonanti ni sauti ambazo hutamkwa kwa kuzuia mkondohewa kutoka mapafuni, ukipitia chemba ya kinywa na chemba ya pua kwenda nje (Kihore na wenzake, 2001). Kiswahili Sanifu kina jumla ya konsonanti 23 zinazotumika katika mfumo lugha wa matamshi na maandishi. Konsonanti hizo ni b, ch, d, dh, f, g, gh, h, j, k, l, m na n. Nyingine ni ny, ng', p, r, s, sh, t, th, v na z. Kwa upande wa Kipemba hali iko tofauti kwa sababu kina konsonanti 29 zinazotumika katika mfumo lugha wa matamshi. Konsonanti hizo ni b, ch, c<sup>h</sup>, d, dh, f, g, gh, h, j, k, k<sup>h</sup>, ky, l, ly, m na n, ny, ng', p, p<sup>h</sup>, r, s, sh, t, t<sup>h</sup>, th, v na z.

#### **4.2.3 Viyeyusho**

Viyeyusho ni sauti ambazo si konsonanti wala si irabu; kwa maana kwamba ni sauti

ambazo huchukuliwa kuwa ziko katikati baina ya irabu na konsonanti. Sauti hizi hazina sifa kamili ya ukonsonanti wala uirabu. Kiswahili Sanifu na lahaja ya Kipemba zina idadi sawa ya viyeyusho viwili; ambavyo ni *y* na *w*. Hata hivyo, kuna tofauti ya matumizi ya sauti hizi, tofauti hizo tutazibainisha katika sehemu zitakazofuata za sura hii.

Kwa ujumla, tunabaini kuwa Kiswahili Sanifu kinatofautiana na lahaja ya Kipemba katika mfumo wa sauti. Kwa mfano, katika Kipemba kuna matumizi ya mpumuo katika sauti  $c^h$ ,  $k^h$ ,  $p^h$  na  $t^h$  ambapo katika Kiswahili Sanifu hakuna mpumuo. Pia, katika Kipemba kuna matumizi ya sauti *ky* na *ly* ambazo hazipatikani katika Kiswahili Sanifu. Kuongezeka kwa sauti hizo sita (6) katika lahaja ya Kipemba kuna ufanya mfumo wa sauti wa lahaja hii uwe na sauti 36 tofauti na mfumo wa Kiswahili Sanifu wenye sauti 30. Hata hivyo, ni vyema kueleza kwamba mfumo wa sauti wa Kipemba cha Kaskazini uko sawa na ule wa Kipemba cha Kusini. Tofauti iliyopo ni matumizi ya sauti hizo kama tutakavyoona katika sehemu inayofuata.

### **4.3 Tofauti za Sauti**

Katika sehemu hii tumejadili na kuchambua lengo mahususi la pili la utafiti huu. Lengo hili linakusudia kubainisha tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Data yetu inaonyesha kuwa kuna tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini katika utamkaji wa baadhi ya maneno. Kwani kuna maneno ambayo wazungumzaji wa Kipemba cha Kaskazini huyatamka tofauti na wazungumzaji wa Kipemba cha Kusini ambapo baadhi ya sauti za neno hubadilishwa kwa kupishana na sauti nyingine. Japokuwa tofauti hizo za

sauti huyafanya maneno yaonekane tofauti kifonetiki lakini maneno hayo huwa na maana sawa au zinazolingana.

#### **4.3.1 Tofauti za Mpishano wa Sauti**

Kuna tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini zinazotokana na mpishano wa sauti katika maneno. Tofauti hizo za mpishano wa sauti zinajidhihirisha katika mpishano wa konsonanti, mpishano wa irabu na mpishano wa nusu-irabu. Aidha, tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini hujibainisha kwa uchopekaji wa sauti, udondoshaji wa sauti na ukakaishaji. Utokeaji wa michakato hiyo unaonekana katika sehemu zitakazofuata hapa chini.

#### **4.3.2 Mpishano wa Konsonanti**

Baadhi ya maneno ya Kipemba cha Kaskazini hutofautiana na yale ya Kipemba cha Kusini katika utamkaji ambapo sauti fulani ya neno hupishana na sauti nyingine. Mpishano huu wa sauti ni mpishano huru kwa sababu haubadilishi maana ya maneno (Besha, 1994). Mpishano ya konsonanti tunayaona katika mpishano wa sauti ni wa sauti [m]:[n], [ch]:[sh], [sh]:[ch], [s]:[sh], [sh]:[s], [j]:[g], [l]:[d], [ky]:[ch] na [r]:[l].

##### **4.3.2.1 Mpishano wa Sauti[m]:[n]**

Kuna tofauti katika utamkaji wa sauti [m] inapotamkwa peke yake kama silabi katika neno baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Wazungumzaji wa Kipemba cha Kusini huitamka sauti [m] ambapo wazungumzaji wa Kipemba cha Kaskazini huitamka [n]. Tuchunguze mifano ifuatayo:-

(1)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>Nke</i>	<i>mke</i>	‘mke’
	<i>nkia</i>	<i>mkia</i>	‘mkia’
	<i>nkono</i>	<i>mkono</i>	‘mkono’
	<i>nlima</i>	<i>mlima</i>	‘mlima’
	<i>nsitu</i>	<i>msitu</i>	‘msitu’

Katika mifano (1) hapo juu tunabaini kuwa mahali pa sauti [m], ambayo ni nazali ya midomo inaposimama peke yake kama silabi katika neno, wazungumzaji wa Kipemba cha Kaskazini hutamka sauti [n], ambayo ni nazali ya ufizi. Hapa tunabaini kuwa kuna mpishano wa sauti hizo baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini.

Kuhusu hali hiyo, uchunguzi wetu tuligundua kuwa baadhi ya wazungumzaji wa Kipemba cha Kusini pia hutamka sauti [n] badala ya [m] kama wanavyotamka wazungumzaji wa Kipemba cha Kaskazini. Kwa mujibu wa utafiti huu watu hao sio wazawa wa maeneo yanayohusika. Kwa mujibu wa Juma (2011) Katika Kipemba nazali ya midomo [m] hubadilika kuwa nazali ya ufizi [n] katika maneno yote ikiwa itafuatiwa na konsonanti isipokuwa konsonanti [p, b, f na v].

#### 4.3.2.2 Mpishano wa Sauti [ch]:[sh]

Pia, kuna tofauti katika utamkaji wa sauti [ch] na [sh] baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Wazungumzaji wa Kipemba cha Kaskazini hutamka sauti [ch] ambapo wazungumzaji wa Kipemba cha Kusini hutamka [sh]. Tuangalie mifano ifuatayo:-

(2)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>chavu</i>	<i>shavu</i>	‘shavu’
	<i>chota</i>	<i>shota</i>	‘chota’
	<i>choto</i>	<i>shoto</i>	‘choto’
	<i>chiriva</i>	<i>shiriva</i>	‘maji chumvi’
	<i>chonga</i>	<i>shonga</i>	‘chonganisha’

Katika mifano (2) tunabaini kuwa katika Kipemba cha Kusini sauti [ch] ambayo ni kizuio-kwamizi kisoghuna cha kaaka gumu hutamkwa sauti [sh] ambayo ni kikwamizi kisoghuna cha kaaka gumu ambapo wazungumzaji wa Kipemba cha Kaskazini hutamka [ch].

#### 4.3.2.3 Mpishano wa Sauti [sh]:[ch]

Aidha, kuna tofauti katika utamkaji wa sauti [sh] na [ch] baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Wazungumzaji wa Kipemba cha Kaskazini hutamka sauti [sh] ambapo wazungumzaji wa Kipemba cha Kusini hutamka [ch]. Tofauti hii ni kinyume cha mwelekeo wa § 4.2.2.2 hapo juu. Tuangalie mifano ifuatayo:-

(3)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>shaza</i>	<i>chaza</i>	‘chaza’
	<i>shawa</i>	<i>chawa</i>	‘chawa’
	<i>shungwa</i>	<i>chungwa</i>	‘chungwa’
	<i>shunvi</i>	<i>chuvi</i>	‘chumvi’
	<i>shushuka</i>	<i>chuchuka</i>	‘chuchuka’

Kupitia mifano (3) tunabaini kuwa katika Kipemba cha Kaskazini sauti [ch] ambayo ni kizuio-kwamizi kisoghuna cha kaaka gumu hutamkwa sauti [sh] ambayo ni kikwamizi kisoghuna cha kaaka gumu ambapo wazungumzaji wa Kipemba cha Kusini hutamka [ch].

#### 4.3.2.4 Mpishano wa Sauti [s]:[sh]

Vilevile, kuna tofauti katika utamkaji wa sauti [s] na [sh] kwa baadhi ya maneno baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Wazungumzaji wa Kipemba cha Kusini huitamka [sh] ambapo wazungumzaji wa Kipemba cha Kaskazini huitamka [s]. Tuchunguze mifano ifuatayo hapa chini:-



(4)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>tapisi</i>	<i>tapishi</i>	‘tapishi’
	<i>mosi</i>	<i>moshi</i>	‘moshi’
	<i>sirikali</i>	<i>shirikali</i>	‘serikali’
	<i>singo</i>	<i>shingo</i>	‘shingo’
	<i>mpisi</i>	<i>mpishi</i>	‘mpishi’

Katika mifano (4) tunabaini kuwa katika Kipemba cha Kaskazini sauti [sh] ambayo ni kikwamizi kisoghuna cha kaakaa gumu, hutamkwa kama sauti [s], ambayo ni kikwamizi kisoghuna cha ufizi, lakini kwa upande wa wazungumzaji wa Kipemba cha Kusini sauti hiyo hutamkwa [sh].

#### 4.3.2.5 Mpishano wa Sauti [sh]:[s]

Kuna tofauti katika utamkaji wa sauti [sh] na [s] kwa baadhi ya maneno baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Wazungumzaji wa Kipemba cha Kaskazini huitamka [sh] ambapo wazungumzaji wa Kipemba cha Kusini huitamka [s]. Tofauti hii ni kinyume cha mwelekeo wa § 4.2.2.4 hapo juu. Tuangalie mifano hapa chini:-

(5)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>matushi</i>	<i>matusi</i>	‘matusi’
	<i>shikio</i>	<i>sikio</i>	‘sikio’
	<i>shindano</i>	<i>sindano</i>	‘sindano’
	<i>shanjari</i>	<i>sanjari</i>	‘sanjari’

Katika mifano (5) tunaona kuwa katika Kipemba cha Kusini sauti [sh] ambayo ni kikwamizi kisoghuna cha kaakaa gumu, hutamkwa kama sauti [s], ambayo ni kikwamizi kisoghuna cha ufizi, lakini kwa upande wa wazungumzaji wa Kipemba cha Kaskazini sauti hiyo hutamkwa [sh].

#### 4.3.2.6 Mpishano wa Sauti [j]:[g]

Kuna tofauti katika utamkaji wa sauti [j] na [g] kwa baadhi ya maneno baina ya

Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Wasemaji wa Kipemba cha Kaskazini huitamka [j] ambapo wasemaji wa Kipemba cha Kusini huitamka [g]. Mifano ifuatayo inadhihirisha:-

(6)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>joma</i>	<i>goma</i>	'joma'
	<i>jani</i>	<i>gani</i>	'jani'
	<i>jina</i>	<i>gina</i>	'jina'
	<i>juba</i>	<i>guba</i>	'juba'

Kupitia mifano (6) tunaweza kuona kuwa katika Kipemba cha Kusini sauti [j], ambayo ni kizuio kwamizi ghuna cha ufizi, hutamkwa sauti [g] ambayo ni kipasuo ghuna cha kaakaa laini ambapo kwa upande wa wasemaji wa Kipemba cha Kaskazini sauti hiyo huitamka (j).

#### 4.3.2.7 Mpishano wa Sauti [l]:[d]

Tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini pia tunaweza kuziona katika utamkaji wa sauti [l] na [d] kwa baadhi ya maneno. Tuchunguze mifano kutoka katika data yetu:-

(7)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>lema</i>	<i>dema</i>	'dema'
	<i>kilevu</i>	<i>kidevu</i>	'kidevu'
	<i>liko</i>	<i>diko</i>	'diko'
	<i>lindi</i>	<i>dindi</i>	'lindi'
	<i>lenga</i>	<i>denga</i>	'lenga'

Kupitia mifano (7) hapo juu tunaona kuwa sauti [d], ambayo ni kipasuo ghuna cha ufizi, hutamkwa hivyo na wasemaji wa Kipemba cha Kusini lakini sauti hiyo hulainishwa na wasemaji wa Kipemba cha Kaskazini kwa kuitamka sauti [l] ambayo ni kitambaza cha ufizi.

#### 4.3.2.8 Mpishano wa Sauti [r]:[l]

Sauti [r] na [l] katika Kiswahili Sanifu hutumiwa kutofautisha maana za maneno yaani sauti moja inapowekwa mahali pa mwenzake maana ya neno hubadilika. Lakini kuna mpishano wa sauti hizi baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini, mpishano huu huwa haubadilishi maana za maneno. Tuchunguze mifano ifuatayo:-

(8)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>birika</i>	<i>Bilika</i>	‘birika’
	<i>urimbo</i>	<i>ulimbo</i>	‘urimbo’
	<i>mwereka</i>	<i>mweleka</i>	‘mwereka’
	<i>kibatari</i>	<i>kibatali</i>	‘kibatari’

Katika mifano (8) hapo juu inatubainishia kuwa sauti [r] ambayo ni kimadende cha ufizi hutumiwa na wasemaji wa Kipemba cha Kaskazini lakini sauti hiyo hubadilishwa na wasemaji wa Kipemba cha Kusini kuwa sauti [l] ambayo ni kitambaza cha ufizi.

#### 4.3.2.9 4.2.2.9 Mpishano wa Sauti [z] : [v]

Kuna tofauti za utamkaji wa sauti [v] na [z] baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Wasemaji wa Kipemba cha Kaskazini hutumia sauti /z/ lakini wasemaji wa Kipemba cha Kusini hutumia sauti /v/ kama tunavyoona katika mifano ifuatayo:-

(9)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>viumbe</i>	<i>ziumbe</i>	‘viumbe’
	<i>vijitu</i>	<i>Zijitu</i>	‘vijitu’
	<i>vijiji</i>	<i>Zijiji</i>	‘vijiji’
	<i>vinu</i>	<i>Zinu</i>	‘vinu’
	<i>vishindo</i>	<i>zishindo</i>	‘vishindo’

Katika mifano (9) tunaona kuwa sauti [z], ambayo ni kikwamizi ghuna cha ufizi, hutumiwa na wasemaji wa Kipemba cha Kusini, lakini sauti hiyo hubadilishwa na

wasemaji wa Kipemba cha Kaskazini kuwa [v] ambayo ni kikwamizi ghuna cha midomo na meno.

### 4.3.3 Mpishano wa Irabu

Mpishano wa irabu katika baadhi ya maneno unatubainishia tofauti nyingine za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Katika utamkaji wa baadhi ya maneno irabu hupishana lakini neno likabaki kuwa na maana ileile kwa Kaskazini na Kusini. Tuzingatie mifano ifuatayo hapa chini:-

(10)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>sarahange</i>	<i>sarahangi</i>	‘sarahangi’
	<i>fetehi</i>	<i>Fetehe</i>	‘mfitinishaji’
	<i>puma</i>	<i>Poma</i>	‘pumua’
	<i>dondo</i>	<i>dundu</i>	‘dondo’

Katika mifano (10) hapo juu tunaona mpishano wa irabu katika utamkaji wa maneno baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Kwa mfano, mpishano wa [e] : [i], mpishano wa [i] : [e], mpishano wa [u] : [o] na mpishano wa [o] : [u]. Kupishana kwa irabu katika maneno hayo kunabainisha tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Ingawa maneno hayo yanatamkwa tofauti kutokana na kutofautiana baadhi ya irabu lakini yana maana sawa.

### 4.3.4 Mpishano wa Nusu-Irabu [w]:[y]

Kuna tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini zinazojitokeza katika mpishano wa nusu-irabu au viyeyusho. Tuangalie mifano ifuatayo:

(11)	KKAS	KKUS	TAFSIRI
	<i>puwa</i>	<i>puya</i>	‘pua’
	<i>funguwa</i>	<i>funguya</i>	‘fungua’
	<i>pwaa</i>	<i>pyaa</i>	‘upwa’
	<i>zinguwa</i>	<i>zunguya</i>	‘zingua’
	<i>vuwa</i>	<i>vuya</i>	‘vua’

Katika mifano (11) tunaona kuwa kuna tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini zinazotokana na mpishano wa nusu-irabu. Kwa mfano, wazungumzaji wa Kipemba cha Kaskazini wanapotamka ‘w’ wazungumzaji wa Kipemba cha Kusini hutamka ‘y’.

#### 4.3.5 Uchopekaji na Udondoshaji wa Sauti

Tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini zinaonekana katika michakato ya uchopekaji na udondoshaji wa sauti. Katika baadhi ya maneno wazungumzaji wa Kipemba cha Kaskazini huchopeka sauti fulani lakini sauti hiyo hudondoshwa na wazungumzaji wa Kipemba cha Kusini na kinyume chake. Katika michakato hiyo kuna uchopekaji na udondoshaji wa [m], [n], [k], [ly], [y] na [kw] kama tutakavyoona katika sehemu zitakazofuata.

##### 4.3.5.1 Uchopekaji na Udondoshaji wa [m]

Kuna tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini zinazotokana na uchopekaji wa [m] katika utamkaji wa baadhi ya maneno ya Kipemba cha Kaskazini lakini sauti hiyo hudondoshwa katika Kipemba cha Kusini.

Tuangalie mifano ifuatayo:

(12)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>Mbingu</i>	<i>bingu</i>	‘mbingu’
	<i>Mvuje</i>	<i>vuje</i>	‘mvuje’
	<i>Mvua</i>	<i>vua</i>	‘mvua’
	<i>Mpira</i>	<i>pira</i>	‘mpira’
	<i>Mfuko</i>	<i>fuko</i>	‘mfuko’

Katika mifano (12) tunabaini kuwa kuna tofauti za kifonolojia katika maneno hayo zitokanazo na uchopekaji wa [m] katika Kipemba cha Kaskazini na udondoshaji wa sauti hiyo katika Kipemba cha Kusini.

#### 4.3.5.2 Uchopekaji na Udondoshaji wa [n]

Kuna tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini zinazotokana na uchopekaji wa [n] katika utamkaji wa maneno ya Kipemba cha Kaskazini lakini sauti hiyo hudondoshwa katika Kipemba cha Kusini. Tuangalie mifano ifuatayo:

(13)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>chenza</i>	<i>cheza</i>	‘chenza’
	<i>funza</i>	<i>fuza</i>	‘funza’
	<i>tunza</i>	<i>tuza</i>	‘tunza’
	<i>penzi</i>	<i>pezi</i>	‘penzi’
	<i>nzuri</i>	<i>zuri</i>	‘nzuri’

Katika mifano (13) tunabaini kuwa kuna tofauti za kifonolojia katika maneno hayo zitokanazo na uchopekaji wa [n] katika Kipemba cha Kaskazini na udondoshaji wa sauti hiyo katika Kipemba cha Kusini.

#### 4.3.5.3 Uchopekaji na Udondoshaji wa [k]

Kuna tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini zinazotokana na uchopekaji wa [k] katika utamkaji wa baadhi ya maneno ya

Kipemba cha Kusini lakini sauti hiyo hudondoshwa katika Kipemba cha Kaskazini.

Tuangularie mifano ifuatayo:

(14)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>Oga</i>	<i>koga</i>	‘oga’
	<i>Osa</i>	<i>kosa</i>	‘osha’
	<i>Omba</i>	<i>komba</i>	‘omba’
	<i>Ondoa</i>	<i>kondoa</i>	‘ondoa’
	<i>Owa</i>	<i>kowa</i>	‘oa’

Katika mifano (14) tunaona kuwa kuna tofauti za kifonolojia katika maneno hayo zitokanazo na uchopekaji wa [k] katika Kipemba cha Kusini na udondoshaji wa sauti hiyo katika Kipemba cha Kaskazini.

#### 4.3.5.4 Uchopekaji na Udondoshaji wa [ly]

Kuna tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini zinazotokana na uchopekaji wa [ly] katika utamkaji wa baadhi ya maneno ya Kipemba cha Kusini lakini sauti hiyo hudondoshwa katika Kipemba cha Kaskazini. Tuangularie mifano ifuatayo:

(15)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>Kaa</i>	<i>kalya</i>	‘kaa’
	<i>Vyaa</i>	<i>vyalya</i>	‘zaa’
	<i>Vaa</i>	<i>valya</i>	‘vaa’
	<i>Anka</i>	<i>lyamka</i>	‘amka’
	<i>Unju</i>	<i>lyunju</i>	‘asubuhi’

Katika mifano (15) tunabaini kuwa kuna tofauti za kifonolojia katika maneno hayo zitokanazo na uchopekaji wa [ly] katika Kipemba cha Kusini na udondoshaji wa sauti hiyo katika Kipemba cha Kaskazini.

#### 4.3.5.5 Uchopekaji na Udondoshaji wa [y]

Kuna tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini zinazotokana na uchopekaji wa [y] katika utamkaji wa baadhi ya maneno ya Kipemba cha Kusini lakini sauti hiyo hudondoshwa katika Kipemba cha Kaskazini.

Tuangalie mifano ifuatayo:

(16)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>Oza</i>	<i>yoza</i>	‘oza’
	<i>dagaa</i>	<i>dagaya</i>	‘dagaa’
	<i>bankuu</i>	<i>bankuyu</i>	‘baba mkubwa’
	<i>okota</i>	<i>yokota</i>	‘okota’
	<i>ungo</i>	<i>yungo</i>	‘ungo’

Katika mifano (16) tunabaini kuwa kuna tofauti za kifonolojia katika maneno hayo zitokanazo na uchopekaji wa [y] katika Kipemba cha Kusini na udondoshaji wa sauti hiyo katika Kipemba cha Kaskazini.

#### 4.3.5.6 Uchopekaji na Udondoshaji wa [kw]

Kuna tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini zinazotokana na uchopekaji wa [kw] katika utamkaji wa baadhi ya maneno ya Kipemba cha Kusini lakini sauti hiyo hudondoshwa katika Kipemba cha Kaskazini. Tuangalie mifano ifuatayo:

(17)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>Imba</i>	<i>kwimba</i>	‘imba’
	<i>Aga</i>	<i>kwaga</i>	‘potea’
	<i>Eleya</i>	<i>kweleya</i>	‘elea’
	<i>Eleka</i>	<i>kweleka</i>	‘beba’

Katika mifano (17) tunabaini kuwa kuna tofauti za kifonolojia katika maneno hayo zitokanazo na uchopekaji wa [kw] katika Kipemba cha Kusini na udondoshaji wa sauti hiyo katika Kipemba cha Kaskazini.



#### 4.3.6 Ukaakaishaji

Massamba (2004) anafasili *ukaakaishaji* kuwa ni utamkaji wa sauti ambao kwao sehemu ya mbele ya ulimi husukumwa nyuma kuelekea kwenye kaaka. Ukakaishaji hufanya sauti isiyo ya kaaka gumu kutamkwa katika mwelekeo wa kaaka gumu. Kwa hiyo, kuna tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini zinazoonekana katika ukaakaishaji. Tuangalie mifano ifuatayo:

(18)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>kyano</i>	<i>chano</i>	‘chano’
	<i>kyuma</i>	<i>chuma</i>	‘chuma’
	<i>kyungu</i>	<i>chungu</i>	‘chungu’
	<i>kyombo</i>	<i>chombo</i>	‘chombo’
	<i>kyuo</i>	<i>chuo</i>	‘chuo’

Katika mifano (18), tunabaini kuwa sauti [ch] ambayo ni kizuio kwamizi kisoghuna cha kaaka gumu hutamkwa kama ilivyo katika Kiswahili Sanifu kwa upande wa Kusini lakini sauti hiyo hutamkwa [ky] ambayo ni kizuio kwamizi kisoghuna cha kaaka laini kwa upande wa Kaskazini.

Pia, katika Kipemba cha Kaskazini kuna ukaakaishaji wa [n] ambao hujitokeza kwa baadhi ya maneno. Tuchunguze mifano ifuatavyo:

(19)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>nyaka</i>	<i>myaka</i>	‘miaka’
	<i>nyendo</i>	<i>myendo</i>	‘miendo’
	<i>nyezi</i>	<i>myezi</i>	‘miezi’
	<i>nyoyo</i>	<i>myoyo</i>	‘mioyo’

Mifano (19) hapo juu inabainisha kuwa ukaakaishaji hutokea pale ambapo sauti [m] ambayo ni nazali ya midomo inapofuatiwa na irabu *i* ambayo pia hufuatiwa na irabu isiyofanana nayo. Wazungumzaji wa Kipemba cha Kaskazini sauti hiyo huitamka [ñ], ambayo ni nazali ya kaaka gumu.

#### 4.3.7 Mchakato wa Mpumuo

Katika Kiswahili Sanifu mpumuo hauonyeshwi kama ni sifa bainifu ya sauti ya lugha hii lakini mpumuo hujitokeza waziwazi katika utamkaji wa vitamkwa [p, k, t na ch] katika lahaja ya Kipemba. Massamba (2004) anafasili *mpumuo* kuwa ni utamkaji wa sauti ambao unaandamana na hewa inayosikika kimlio. Mpumuo hubainisha tofauti nyingine ya kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Tuchunguze mifano ifuatayo:

(20)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>kamba</i>	<i>k'amba</i>	'kamba'
	<i>chana</i>	<i>ch'ana</i>	'chana'
	<i>utembo</i>	<i>ut'embo</i>	'utembo'
	<i>Taa</i>	<i>t'aa</i>	'taa'
	<i>Paa</i>	<i>p'aa</i>	'paa'

Katika mifano (20), tunaona kuwa kuna tofauti za kifonolojia zinazotokana na mpumuo kwa baadhi ya maneno baina Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Licha ya matumizi tofauti ya mpumuo, maneno tuliyoyabainisha katika mifano hapo juu yana maana sawa baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini.

#### 4.4 Tofauti za Kimofolojia

Katika sehemu hii tumejadili lengo letu mahususi la tatu ambalo linataka kulinganisha tofauti za kimofolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Vipengele vya kimofolojia vilivyojadiliwa katika sehemu hii ni mofolojia ya nomino na kitenzi baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Pia, sehemu hii inabainisha na kujadili vipashio vya kisarufi ambapo kwa kiasi kikubwa imejikita katika mofolojia na baadhi ya vipengele vya kimiundo. Kwa maneno mengine, hapa tumeichukulia mofolojia kama mchakato na sintaksia kama mofolojia tendeshi. Hii

ni kwa sababu baadhi ya wakati katika isimu ya lugha ni vigumu kutofautisha maumbo ya kimofolojia bila kutumia mifano ya miundo ya kisintaksia hasa katika kiwango cha uchambuzi.

#### 4.4.1 Mofolojia ya Nomino

Katika uchambuzi wetu tumejihusisha na ngeli za nomino. Kwa kweli vipashio hivi vina dhima kubwa zaidi kikazi kuliko kisemantiki. Kwa ufupi sana tumechambua baadhi ya viambajengo vya kimofolojia na kisarufi kwa kuangalia uhusiano wa viambishi vya maneno na baadhi ya miundo ya kisintaksia kila ilipolazimu kufanya hivyo.

**Jedwali na. 4.1: Ngeli za Nomino**

Ngeli	Kiambishi Awali Ngeli		Kipemba cha Kaskazini		Kipemba cha Kusini	
	Umoja	Wingi	Umoja	Wingi	Umoja	Wingi
1/2	<i>n-/</i>	<i>wa-</i>	<i>ntu</i>	<i>watu</i>	<i>mtu</i>	<i>Watu</i>
	<i>m-</i>		<i>mvulyana</i>	<i>wavulyana</i>	<i>mvulyana</i>	<i>wavulana</i>
	<i>mu-</i>		<i>muume</i>	<i>waume</i>	<i>mu yume</i>	<i>wayume</i>
	<i>mw-</i>		<i>mwana</i>	<i>wana</i>	<i>mwana</i>	<i>Wana</i>
3/4	<i>n-/</i>	<i>mi-</i>	<i>nti</i>	<i>miti</i>	<i>mti</i>	<i>Miti</i>
	<i>m-</i>		<i>mpapai</i>	<i>mi papai</i>	<i>mpapayi</i>	<i>mi papayi</i>
	<i>mu-</i>		<i>mwembe</i>	<i>miembe</i>	<i>muwembe</i>	<i>miyembe</i>
	<i>mw-</i>		<i>mwanzi</i>	<i>mi(y)anzi</i>	<i>mwanzi</i>	<i>miyanzi</i>
5/6	<i>ji-</i>	<i>ma-</i>	<i>jimbi</i>	<i>majimbi</i>	<i>jimbi</i>	<i>majimbi</i>
	<i>ø-</i>		<i>øfuti</i>	<i>mafuti</i>	<i>øgoti</i>	<i>Magoti</i>
	<i>i-</i>		<i>ipu</i>	<i>mapu</i>	<i>jipu</i>	<i>Majipu</i>
	<i>zi-</i>		<i>zicho</i>	<i>macho</i>	<i>dicho</i>	<i>Macho</i>
7/8	<i>ki-</i>	<i>vi-</i>	<i>kiwatu</i>	<i>viwatu</i>	<i>kiyatu</i>	<i>Ziyatu</i>
	<i>ky-</i>	<i>vy-</i>	<i>kyano</i>	<i>vyano</i>	<i>chano</i>	<i>Vyano</i>
9/10	<i>n-</i>	<i>n-</i>	<i>nshi</i>	<i>nshi</i>	<i>øchi</i>	<i>Øchi</i>
11/10a	<i>U</i>	<i>n</i>	<i>ulimi</i>	<i>ndimi</i>	<i>lyulimi</i>	<i>Ndimi</i>
12/13	<i>*ka-</i>	<i>*tu-</i>	-	-	-	-
14/6a	<i>u-</i>	<i>ma-</i>	<i>ugonjwa</i>	<i>magonjwa</i>	<i>ugonjwa</i>	<i>magonjwa</i>
15	<i>ku-</i>	<i>ku-</i>	<i>kuvyaa</i>	-	<i>kuvyalya</i>	-
16	<i>pa-</i>	<i>mwa-</i>	<i>pahali</i>	<i>mwahali</i>	<i>pahala</i>	<i>mwahala</i>
17	<i>kwa-</i>		<i>kwahali</i>		<i>kwahala</i>	
18	<i>ma-</i>		<i>mahali</i>		<i>mahala</i>	

Chanzo: Data ya Uwandani 2015

Ngeli za nomino katika Kiswahili zimebainishwa na kujadiliwa na wataalamu mbalimbali kwa mitazamo tofauti. Hata hivyo, utafiti huu umejipusha na mitazamo na mijadala kuhusu aina na migawanyo ya ngeli kwa sababu kufanya hivyo ni kwenda nje ya malengo yetu. Tulichokifanya sisi ni kuwasilisha ngeli halisi na viambishi vyake kama tulivyozipata kutoka katika data yetu. Jedwali lifuatalo linaonyesha ngeli za nomino na viambishi awali vya nomino na vitenzi katika Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini:

#### 4.4.1.1 Tofauti za Viambishi Awali vya Nomino

Katika data yetu tunabaini kuwa mfumo wa ngeli baina ya Kipemba cha Kaskazini hautofautiani sana na mfumo wa ngeli wa Kipemba cha Kusini. Tofauti kubwa inajibainisha katika viambishi awali vya nomino kwa baadhi ya maneno. Tuchunguze mifano hapa chini:

(21)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>	<b>NGELI</b>
	<i>ntu/watu</i>	<i>mtu/watu</i>	‘mtu/watu’	1/2
	<i>zicho/macho</i>	<i>dicho/macho</i>	‘jicho/macho’	5/6
	<i>kyano/vyano</i>	<i>chano/vyano</i>	‘chano/vyano’	7/8
	<i>nshi/nshi</i>	<i>øchi/chi</i>	‘nchi/nchi’	9/10

Katika mifano (21) tunaona tofauti za viambishi awali umoja vya maneno vilivyokolezwa baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Hata hivyo, ni vyema ieleweke kwamba tofauti hizi ndio zile tofauti za kifonolojia ambazo tumezijadili kwa mifano kuanzia § 4.2.1 hadi § 4.2.5 katika tasnifu hii.

#### 4.4.1.2 Uhamaji wa Ngeli

Baadhi ya lugha za Kibantu zina unyumbufu wa ngeli, kwa maana kwamba baadhi ya nomino huhama kutoka ngeli moja kwenda nyingine (Kihore na wenzake, 2001).

Pia, tumegundua kwamba katika Kipemba cha Kaskazini baadhi ya nomino zina tabia ya kuhama kutoka kundi moja kwenda kundi jingine ambapo nomino hizo hubakia katika kundi lake katika Kipemba cha Kusini.

Katika Kipemba cha Kusini, kwa mfano, nomino zote zinazohusu viumbe vyenye uhai na hisivu, zinaingia katika kundi 1/2. Lakini katika Kipemba cha Kaskazini kuna baadhi ya nomino ambazo huhamishiwa katika ngeli ya 9/10. Tuangalie mifano michache ifuatayo:

(22)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>	<b>NGELI</b>
	<i>ng'ombe</i>	<i>ng'ombe</i>	<i>ng'ombe</i>	1/2
	<i>nyuki</i>	<i>nyuki</i>	<i>Nyuki</i>	1/2

Uhamaji huo kutoka kundi moja la ngeli kwenda kundi jingine unabainika katika kiwango cha kisintaksia. Tuangalie sentensi zifuatazo hapa chini:

- (a) *Ng'ombe in'chinjwa*  
‘Ng'ombe amechinjwa’
- (b) *Ng'ombe zin'chinjwa*  
‘Ng'ombe wamechinjwa’
- (c) *Nyuki in'niuma*  
*Nyuki ameniuma*
- (d) *Nyuki zin'niuma*  
‘Nyuki wameniuma’

Mifano (a-d) hapo juu inabainisha kuwa katika Kipemba cha Kaskazini kuna uhamishaji wa baadhi ya nomino za viumbe vyenye uhai na hisivu kutoka kundi la 1/2 (a – wa) kwenda kundi la 9/10 (i – zi). Hii inatokana na ukweli kwamba baadhi

ya lugha za Kibantu zina unyumbufu wa ngeli, kwa maana kwamba baadhi ya nomino huhama kutoka ngeli moja kwenda nyingine.

#### 4.4.2 Mofolojia ya Kitenzi

Kitenzi ni neno linaloarifu jambo linalofanywa na mtu, mnyama, au kitu kingine chochote (Habwe na Karanja, 2004). Kitenzi cha Kiswahili kama lugha nyingine za Kibantu huongezewa viambishi mwanzoni na mwishoni ambavyo hukifanya kitenzi hicho kiweze kubadilika. Kuna tofauti za viambishi vya kitenzi baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini katika mofolojia ya kitenzi. Tofauti hizo tumezigundua katika viambishi vya mtenda, njeo na kauli, miishio ya baadhi ya vitenzi na vitenzi vishirikishi.

##### 4.4.2.1 Viambishi vya Mtenda

Kuna tofauti za viambishi awali vya mtenda vya nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu umoja baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini ambapo kiambishi kimoja kinaweza kuwa na maumbo mbalimbali. Viambishi vinavyotofautiana ni vile vya umoja tu na hutofautiana katika hali ya uyakinishi pekee. Tuchunguze jedwali lifuatalo:

**Jedwali na. 4.2: Viambishi vya Mtenda**

Nafsi	Kipemba cha Kaskazini	Kipemba cha Kusini	Kisanifu
	n(i)- hi- ka-	ho- he- ha-	ni-
	u- we- ku-	ku-	u-
	a- yu- ka-	ka-	a-

Chanzo: Data ya Uwandani 2015

#### 4.4.2.1.1 Viambishi vya Mtenda Nafsi 1

Kwa mujibu wa jedwali na. 4.2 kuna tofauti za maumbo ya kiambishi awali cha mtenda nafsi ya kwanza umoja uyakinishi. Tuangalie mifano ifuatayo:

(23)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>nkiota</i>	<i>hota</i>	‘nikiota’
	<i>hishalima</i>	<i>heshalima</i>	‘nikishalima’
	<i>hawose</i>	<i>hawaoze</i>	‘nikawaoshe’

Katika mifano (23) tunaona kuwa kiambishi awali cha mtenda nafsi ya kwanza katika Kipemba cha Kaskazini kina maumbo matatu; *n-*, *hi-* na *ha-* lakini katika Kipemba cha Kusini viambishi hivyo huwakilishwa na maumbo *h-*, *he-* na *ha-*.

#### 4.4.2.1.2 Viambishi vya Mtenda Nafsi 2

Pia kuna tofauti za maumbo ya viambishi awali vya mtenda nafsi ya pili umoja baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Tuangalie data kupitia mifano:

(24)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>Utavuwa</i>	<i>kutavuya</i>	‘utavua’
	<i>Wavuwa</i>	<i>kunavuya</i>	‘unavua’
	<i>Wevuwa</i>	<i>kuvuyi</i>	‘ulivua’
	<i>Kunvuwa</i>	<i>kumuvuya</i>	‘umevua’

Mifano (24) inadhihirisha kuwa maumbo ya viambishi awali mtenda nafsi ya pili katika Kipemba cha Kaskazini ni *u-*, *wa*, *we-* na *ku-* ambapo katika Kipemba cha Kusini huwakilishwa na umbo *ku-*.

#### 4.4.2.1.3 Viambishi vya Mtenda Nafsi 3

Aidha, kuna tofauti za viambishi vya mtenda nafsi ya tatu umoja baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Tofauti hizo ni hizi zifuatazo:

(25)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>Asoma</i>	<i>kanasoma</i>	‘anasoma’
	<i>Yuasoma</i>	<i>kanasoma</i>	‘yuasoma’
	<i>Esoma</i>	<i>kasomi</i>	‘alisoma’
	<i>Kasomo</i>	<i>kamasoma</i>	‘amesoma’

Katika mifano (25) tunaona kuwa viambishi vya mtenda nafsi ya tatu umoja katika Kipemba cha Kaskazini huwakilishwa na maumbo; *a-*, *yu-*, *e-* na *ka-* ambapo katika Kipemba cha Kusini viambishi hivyo huwakilishwa na umbo *ka-*.

#### 4.4.3 Maumbo ya Njeo

Katika sehemu hii tutaziangalia mofimu za njeo<sup>2</sup> ambazo huwekwa kabla ya mzizi wa kitenzi. Lahaja za Kipemba cha Kaskazini na Kusini kama kilivyo Kiswahili Sanifu, nazo zina njeo tatu; yaani njeo ya wakati uliopita, uliopo na ujao. Kwa hivyo, tumezichunguza tofauti za njeo hizo na kuzibaini katika hali ya uyaakinishi.

##### 4.4.3.1 Njeo ya Wakati uliopita

Kuna tofauti ya mofimu za kuonyesha wakati uliopita baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Wasemaji wa Kaskazini hutumia mofimu **-e-** ambapo Wasemaji wa Kusini hutumia mofimu **-li-**. Tuchunguze mifano ifuatayo:

(26)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>Nepika</i>	<i>nilipika</i>	‘nilipika’
	<i>Twekubali</i>	<i>tulidumba</i>	‘tulikubali’
	<i>Wesikiya</i>	<i>ulisikili</i>	‘ulisikia’
	<i>Mwesikia</i>	<i>mlisikili</i>	‘mlisikia’
	<i>Etongowa</i>	<i>alitongola</i>	‘alisema’
	<i>Wefika</i>	<i>walifika</i>	‘walifika’

<sup>2</sup> Njeo ni kipengele cha kisarufi kinachoonyesha uhusiano kati ya nafasi mbili za wakati. Mara nyingi dhana hii hugawanywa katika nyakati tatu kuu: wakati uliopo, wakati uliopita na wakati ujao.



Kupitia mifano (26) hapo juu tunabaini kuwa mofimu ya wakati uliopita katika Kipemba cha Kaskazini ni *-e-* ambapo wasemaji wa Kusini hutumia *-li-* kama ilivyo katika Kiswahili Sanifu.

#### 4.4.3.1.1 Njeo ya Wakati Uliopo

Kuna tofauti ya kueleza wakati uliopo kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini ambapo wasemaji wa Kipemba cha Kaskazini hutumia mofimu *-Ø-* na wasemaji wa Kusini hutumia mofimu *-ma-*. Mifano ifuatayo inaweka bayana:

(27)	KKAS	KKUS	TAFSIRI
	<i>naØ ja</i>	<i>nimakuja</i>	‘ninakuja’
	<i>waØlya</i>	<i>wamalya</i>	‘anakula’
	<i>aØfuwa</i>	<i>kamafuya</i>	‘anafua’
	<i>waØlala</i>	<i>kumalala</i>	‘unalala’

Pia, Kipemba cha Kaskazini wakati mwingine hutumia *-ke-* kwa wakati uliopo kuonyesha kitendo kinachoendelea kufanyika ambapo katika Kusini hutumia *-ngali-*.

Mifano:

(28)	KKAS	KKUS	TAFSIRI
	<i>Ikeshanga</i>	<i>ingalichanga</i>	‘ingalichanga’
	<i>wakewadigi</i>	<i>wangaliwaduchu</i>	‘wangaliwadogo’
	<i>Tukesoma</i>	<i>tungalisoma</i>	‘tungalisoma’

Sambamba na mifano hiyo, wakati mwingine wasemaji wa Kipemba cha Kaskazini hutumia *-kali-* ambayo ina dhima sawa na *-ke-* iliyopo katika mifano (28) hapo juu.

Aidha, kuna tofauti ya kudhihirisha wakati uliopo katika hali ya kuendelea. Watu wa Kaskazini hutumia *a-* na watu wa Kusini hutumia *hu-*. Mifano:

(29)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>Alya</i>	<i>hulya</i>	‘hula’
	<i>Apita</i>	<i>hupita</i>	‘hupita’
	<i>Acheza</i>	<i>hucheza</i>	‘hucheza’
	<i>Waimba</i>	<i>huimba</i>	‘huimba’

Katika mifano (29) hapo juu tunabaini tofauti za maumbo ya mofimu zinazojidhihirisha kuonesha wakati uliopo katika hali ya kuendelea. Watu wa Kaskazini hutumia *a-* na watu wa Kusini hutumia *hu-*

#### 4.4.3.1.2 Njeo ya Wakati Ujao

Kuna tofauti ya mofimu za kuonyesha wakati ujao baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Katika Kipemba cha Kaskazini hutumia mofimu *-t'a-* yenye mpumuo ambapo katika Kipemba cha Kusini hutumika *-ta-* iso mpumuo. Tuangalie mifano ifuatayo:

(30)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>t'anipa</i>	<i>kutanipa</i>	‘utanipa’
	<i>mut'alala</i>	<i>mtalala</i>	‘mtalala’
	<i>wat'aimba</i>	<i>wataimba</i>	‘wataimba’
	<i>ut'aleta</i>	<i>kutaleta</i>	‘kutaleta’

Katika mifano (30) hapo juu tunaona kuwa Kipemba cha Kaskazini kiambishi awali cha mtenda hakiko wazi wakati katika Kusini kinajidhihirisha wazi wazi. Hivyo *t'* hutumika kubeba dhima ya kiambishi cha mtenda ambacho hakiko wazi.

#### 4.4.4 Miishio ya Vitenzi

Kuna tofauti za maumbo ya miishio ya baadhi ya vitenzi baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Katika Kipemba cha Kaskazini sauti *-I-* huchopekwa katika kitenzi kuonyesha wakati uliopita kwa kitendo kilichokamilika. Tuangalie mifano:

(31)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>Kakimbili</i>	<i>kamakimbiya</i>	‘alikingibia’
	<i>Kawapikili</i>	<i>kawapikiya</i>	‘aliwapikia’
	<i>wawanunulili</i>	<i>wawanunuliya</i>	‘waliwanunulia’
	<i>Tuwaombeli</i>	<i>tuliwaombeya</i>	‘tuliwaombea’

Katika mifano (31) hapo juu tunabaini tofauti za maumbo ya mwishoni mwa vitenzi ambapo katika Kipemba cha Kaskazini huchopeka *-l-* na Kusini hutumia *-y-*.

#### 4.4.5 Tangamano Irabu

Kuna tofauti za tangamano irabu baadhi ya vitenzi baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Katika Kipemba cha Kaskazini baadhi ya vitenzi huishia na kiambishi tamati *-a* ambapo katika Kipemba cha Kusini huishia na *-i*. Mifano:

(32)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>Hadaiwa</i>	<i>hadaiwi</i>	‘hadaiwi’
	<i>sielewa</i>	<i>sielewi</i>	‘sielewi’
	<i>Husikiwa</i>	<i>husikiwi</i>	‘husikiwi’

Kwa mujibu wa Nurse (1982:178) hali hiyo ni *tangamano irabu*<sup>3</sup> ambapo katika Kiswahili Sanifu tangamano irabu huishia na kiambishi tamati *-i*. Katika Kipemba cha Kusini hali hiyo ni kama ilivyo katika Kisanifu. Lakini katika Kipemba cha Kaskazini huishia na kiambishi *-a*.

Pia kuna baadhi ya vitenzi katika Kipemba cha Kaskazini huchopekwa *-l-* katika silabi ya mwisho ambapo katika Kipemba cha Kusini vitenzi hivyo silabi ya mwisho huishia na irabu pekee. Mifano:

<sup>3</sup> Hali ya irabu zinazokaribiana kuweza kufanana au kuathiria kwa namna fulani. Zaidi taz. Massamba (2004) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam. TUKI. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

(33)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>Sisikili</i>	<i>sisikiyi</i>	sisikii
	<i>Hunambili</i>	<i>hunambiyi</i>	hunambii
	<i>Hasogeli</i>	<i>hasogeyi</i>	hasogei

Kutokana na mifano (33) tumeweza kubaini kuwa katika Kipemba cha Kaskazini **-I-** huchopekwa katika kitenzi kilichoishia na irabu mbili kuonyesha wakati uliopo katika hali ya ukanushi. Vilevile, katika Kipemba cha Kaskazini **-I-** kama hiyo huchopekwa katika kitenzi kuonyesha wakati uliopita na kitendo kilichokamilika.

Tuangalie mifano ifuatayo:

(34)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>Kakimbili</i>	<i>kanakimbiya</i>	‘alikingia’
	<i>Kawapikili</i>	<i>kanawapikiya</i>	‘aliwapikia’
	<i>Kangili</i>	<i>kanaingiya</i>	‘aliingia’

Kutokana na mifano (33) na (34) hapo juu mbali ya kuonyesha wakati fulani, pia **-I-** ina uamilifu wa kulinda usilabi wa Kibantu yaani KIKI katika Kipemba cha Kaskazini.

#### 4.4.6 Kauli za Kitenzi

Kwa hakika hakuna tofauti kubwa katika kauli za vitenzi baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Hata hivyo, kuna tofauti katika kauli ya usababishi kwa baadhi ya maneno ya Kipemba cha Kaskazini ambayo hutumia **-s-** au **-z-** ambapo Kipemba cha Kusini hutumia **-sh-**. Tuangalie mifano ifuatayo:

(35)	<b>KKAS</b>	<b>KKUS</b>	<b>TAFSIRI</b>
	<i>Wasa</i>	<i>washa</i>	washa
	<i>apisa</i>	<i>apisha</i>	apisha
	<i>Fananiza</i>	<i>fananisha</i>	fananisha
	<i>Sahauliza</i>	<i>sahaulisha</i>	sahaulisha

Katika mifano (35) tunathibitisha kuwa kuna tofauti katika kauli ya usababishi kwa baadhi ya maneno ya Kipemba cha Kaskazini ambayo hutumia *-s-* au *-z-* ambapo Kipemba cha Kusini hutumia *-sh-*.

#### **4.5 Hitimisho la Sura**

Katika sura hii tumechambua na kuwasilisha data zinazohusu tofauti za kifonolojia na kimofolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini zilizokusanywa kutoka uwandani. Katika uchambuzi huu tuliukilia kuchambua malengo mahususi ya utafiti wetu. Hivyo basi, sura hii imebainisha sauti za Kiswahili sanifu na sauti za lahaja ya Kipemba, imebainisha na kujadili tofauti za kifonolojia na kimofolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Sura inayofuata inaelezea muhtasari wa mjadala, hitimisho na mapendekezo.

## SURA YA TANO

### 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 5.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea vipengele kama vile muhtasari wa ugunduzi wa utafiti, kujibu maswali ya utafiti, mchango wa utafiti, hitimisho na mapendekezo kuhusu maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

#### 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Katika sehemu hii tumeeleza muhtasari wa mjadala kuhusu utafiti. Tumeanza kwa kufafanua muhtasari wa jumla, muhtasari wa utafiti, kujibu maswali ya utafiti na mchango wa utafiti. Ufafanuzi wa vipengele hivyo unaonekana katika sehemu zifuatazo hapa chini.

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini, lahaja ambazo zinazungumzwa katika kisiwa cha Pemba. Utafiti huu ulikusudia kufikia malengo mahususi matatu. Lengo la kwanza, kubainisha sauti za lugha ya Kiswahili Sanifu na lahaja ya Kipemba. Pili, kubainisha tofauti za kifonolojia na kimofolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Tatu, kujadili sababu zilizosababisha tofauti za kifonolojia na kimofolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini.

Uchambuzi wa tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini na mjadala wa utafiti umefanywa kwa kutumia nadharia ya *Isimu Historia na*

*Linganishi.* Nadharia hii imetumika ili kulinganisha na kulinganua mofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini ili kuibua tofauti zilizopo.

Kupitia nadharia hii hatimaye tumeweza kubainisha, tofauti za kifonolojia na kimofolojia baina ya lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Nadharia hii ni faafu kwa kulinganisha lugha au lahaja mbili au zaidi zenye uhusiano wa kinasaba yaani zinazotokea kwenye asili moja.

### **5.2.1 Muhtasari wa Utafiti**

Sura ya kwanza imeeleza vipengele vinavyotoa taarifa za awali za utafiti kama vile jiografia ya mahali pa utafiti, usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wa vikwazo na kumalizia kwa hitimisho la sura.

Sura ya pili imebainisha na kujadili mapitio ya kazi tangulizi. Katika kujadili kazi hizo ambazo zimetumika kwenye utafiti huu tumeelezea tafiti za lahaja kwa ujumla na tafiti za lahaja za Kiswahili. Pia sura hii inaelezea kiunzi cha nadharia kilichoongoza utafiti huu na mwisho ni hitimisho la sura.

Sura ya tatu imeeleza na kufafanua mbinu za utafiti ambazo mtafiti alizitumia katika mchakato mzima wa utafiti huu. Vipengele ambavyo vimebainishwa ni muundo wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, sampuli na mbinu ya uteuzi wa sampuli, mbinu za ukusanyaji wa data. Pia, tumeelezea mbinu za uchambuzi wa data uwasilishaji, maadili ya utafiti na hitimisho la sura.

Sura ya nne imechambua na kuwasilisha data zinazohusu tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini zilizokusanywa kutoka uwandani. Katika uchambuzi huo tuliukilia kuchambua malengo mahususi ya utafiti ambapo tumebainisha sauti za Kiswahili na za lahaja ya Kipemba, tofauti za kifonolojia na kimofolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini.

Sura ya tano imeelezea muhtasari wa mjadala wa utafiti. Vipengele vilivyojadiliwa ni muhtasari wa utafiti, kujibu maswali ya utafiti, mchango wa utafiti, hitimisho na mapendekezo kuhusu maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

### **5.2.2 Kujibu Maswali ya Utafiti**

Katika mchakato wa kubainisha, kueleza na kujadili tofauti za kifonolojia na kimofolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini, pia tulijielekeza kujibu maswali ya utafiti (taz. § 1.5) ambayo msingi wake ni malengo mahususi ya utafiti huu (taz. § 1.4.2). Maswali hayo yalikuwa kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza lilikuwa: *Lugha ya Kiswahili Sanifu na lahaja ya Kipemba zina sauti zipi?* Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa lugha ya Kiswahili Sanifu ina sauti za irabu; a, e, i, o na u; viyeyusho w na y na konsonanti, b, ch, d, dh, f, g, gh, h, j, k, l, m, n, ny, ng', p, r, s, sh, t, th, v na z. Kwa upande wa Kipemba nayo ina sauti za irabu; a, e, i, o na u; viyeyusho w na y na konsonanti, b, ch, c<sup>h</sup>, d, dh, f, g, gh, h, j, k, k<sup>h</sup>, ky, l, ly, m na n, ny, ng', p, p<sup>h</sup>, r, s, sh, t, t<sup>h</sup>, th, v na z. Tofauti za sauti hizi tumezibainisha katika § 4.1.



Swali la pili lilikuwa: *Kuna tofauti gani za kifonolojia zinazojibainisha baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini?* Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa kuna tofauti kadhaa za kifonolojia zinazojitokeza baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Miongoni mwa tofauti za kifonolojia ni mpishano wa sauti, uchopekaji na udondoshaji wa sauti, ukaakaishaji na mpumuo. Tofauti hizi tumezibainisha na kuzijadili kwa kina katika § 4.2.1 hadi 4.2.7 katika tasnifu hii.

Kwa hivyo, tumebaini kuwa kuna tofauti za kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Hata hivyo, data yetu imebainisha kwamba tofauti hizo za kifonolojia zinajibainisha zaidi katika baadhi ya maneno na wala sio kwa maneno yote yanayotumika katika mfumo mzima wa lugha.

Swali la tatu lilikuwa: *Kuna tofauti gani za kimofolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini?* Majibu ya swali hili yameelezwa kwa kina katika § 4.3 ya tasnifu hii. Tofauti za kimofolojia zilizoibainisha katika utafiti huu ni katika ngeli za nomino kwenye viambishi awali vya mtenda na uhamaji wa ngeli. Tofauti nyingine zimejibainisha katika mofolojia ya kitenzi kama vile viambishi vya mtenda, njeo, miishio ya baadhi ya vitenzi, tangamano irabu na kauli ya usababishi.

### **5.2.3 Mchango wa Utafiti**

Kwa hakika, utafiti huu una mchango mkubwa katika taaluma ya isimu na maendeleo ya taaluma za lahaja za Kiswahili hususani kwa lahaja ya Kipemba. Kwanza, unatoa mchango wa kubainisha sauti za lahaja ya Kipemba kwa kubainisha

idadi ya sauti 36 ambazo ni irabu 5, viyeyusho 2 na konsonanti 29. Pili, utafiti huu umebainisha tofauti za kifonolojia zinazojibainisha katika lahaja ya Kipemba kwa wazungumzaji wa Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Tatu, utafiti huu unachangia kubainisha na kujadili tofauti za kimofolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Kwa ujumla utafiti huu utakuwa chachu ya watafiti wengine kufanya uchunguzi zaidi wa vipengele vya kiisimu katika Kipemba.

### **5.3 Hitimisho**

Utafiti huu umejaribu kutoa uchunguzi wa awali kuhusu tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini katika kisiwa cha Pemba. Ingawa kuna tofauti za kifonolojia na kimofolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini ambazo pia zinatofautiana na Kiswahili Sanifu kuna mambo kadhaa tunaweza kujiuliza.

Kwanza, tunaweza kujiuliza ni kwa nini Kipemba cha Kaskazini kinatofautiana kwa kiasi fulani kifonolojia na kimofolojia na Kipemba cha Kusini? Kwa mwelekeo huo, je katika kisiwa cha Pemba kuna lahaja zaidi ya moja? Kwa kuwa tumeshasema kuwa utafiti zaidi unahitajika, maswali hayo hayahitaji majibu ya moja kwa moja. Utafiti wa kina zaidi ufanyike ambao utabainisha tofauti nyingine zaidi za fonolojia ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Kwa hivyo, tunategemea kwamba utafiti huu utawafanya watu wengine waanze kuchunguza kwa kina zaidi tofauti kuhusu asili na chimbuko la Kipemba cha Kaskazini na kile cha Kusini. Uchunguzi wa chimbuko utaweza kusaidia kugundua asili ya lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini.

#### **5.4 Mapendekezo kwa ajili ya Tafiti Zaidi**

Kwa hakika, utafiti huu haukutosheleza kila kitu katika eneo lililochunguzwa kwa sababu umechunguza vipengele mahususi na vichache sana vya fonolojia na mofolojia. Hivyo basi, unaweza kuchukuliwa kama ni hatua ya awali ya kupambanua tofauti za kimofonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini. Kwa mantiki hiyo, tunapendekeza kwamba vipengele vingi zaidi vya kiisimu vinahitaji kuchunguzwa kwa kulinganisha na kulinganua lahaja za maeneo haya. Miongoni mwa vipengele hivyo ni sintaksia, na msamiati. Aidha, mada nyingine ambazo zinapendekezwa kuchunguzwa zaidi ni pamoja na asili na chimbuko la Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Pia utafiti unahitajika kulinganisha lahaja za maeneo mbalimbali katika vijiji vya Kaskazini na Kusini vya Kisiwa cha Pemba ili kubaini tofauti na mfanano wa Kipemba katika maeneo mbalimbali ya Kisiwa cha Pemba.

### MAREJELEO

- Adam, J. & Kamuzoro, F. (2007). *Research Methods for Business and Social Studies*  
Morogoro: Mzumbe Book Project.
- Adewole, S. M. (1984). "Agreement as a Cohesive Device in Kiswahili",  
Unpublished M.A. Dissertation, University of Dar es Salaam.
- Anttila, R. (1972). *An Introduction to Historical and Comparative Linguistics*. New  
York: Macmillan Publishing Co. Inc.
- BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.
- Batibo, H. M. (1982). "Mawazo ya Mwanzo kuhusu Uhusiano wa Lahaja za Kusini"  
(Makala ya Semina) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Besha, R. M. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*, Dar es Salaam: Macmillan  
Aidan Ltd.
- Chiraghdin, S. & Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford  
University Press.
- Cohen, L., L. Manion & Morrison, K. (2000). *Research Methods in Education*. Toleo  
la 8. London: Rutledge Falmer.
- Crystal, D. (1985). *Linguistics*. London: Penguin.
- Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix  
Publishers Ltd.
- Ingrams, W. H. (1924). "The Dialects of the Zanzibar Sultanate" in *Bulletin of the  
School of Oriental and African Studies, Vol.III, Part III*, London, uk. 533-  
550.
- Johnston, H. H. (1922). *A Comparative Study of Bantu and Semi-Bantu Languages*  
(Juz.II). Clarendon: Oxford University Press.

- Juma, H. K. (2011). “Tofauti za Kiisimu baina ya Kiswahili cha Micheweni na Wete katika Kisiwa cha Pemba”, Tasnifu ya M. A Kiswahili (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Khamis, S. A. (1984). Urban Versus Rural Swahili, A study of Pemba Varieties Tasnifu Uzamili (haijachapishwa) Leipzig Karl Marks University.
- Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B. & Msajila, Y. P. (2001). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanfu (SAMAKISA), Sekondari na Vyuo*, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- King’ei, K. (2010). *Misingi ya Isimujamii*, Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.
- Kipacha, A. (2003). *Lahaja za Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria. Dar es Salaam: KIUTA.
- Kortmann, B. (2003). “Comparative English Dialect Grammar: A Typological Approach”. In I. M. Palacios/M. J. Lopez Couso/P. Fra/E. Seoane, eds. *Fifty Years of English Studies in Spain (1952:2002)*.
- Kothari, C. (2009), research Methodology, New Delhi: New Age International (P) Limited.
- Ladefoged, P. (1975). *Elements of Acaustic Phonetics*. Chicago: University of Chicago Press.
- Lambert, H. E. (1957). *Kivumba: A Dialect of the Southern Swahili Coast*. Kampala: East African Swahili Committee.
- Lambert, H. E. (1958). *Chi-chifundi: A Dialect of the Southern Swahili Coast*. Kampala: East African Swahili Committee.
- Lass, R. (1984). *Phonology*. New York: Cambridge Press.

- Maganga, C. (1991). "A Study of Morphophonology of Standard Kiswahili, Kipemba, Kitumbatu and Kimakunduchi". Tasnifu ya Uzamivu (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Massamba, D. P. B. (2002). *Historia ya Kiswahili: 50BK hadi 1500BK*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Massamba, D. P. B. (2004) *Kamusi Ya Isimu Na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Massamba, D. P. B. (2006). "Kiswahili cha Musoma: Mwanzo wa Lahaja Nyingine?" katika Kiswahili: *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili* Juzuu ya 69 uk 37-59, Dar es Salaam: Dar es Slaam University Press.
- Massamba, D. P. B. (2007). *Kiswahili Origins and Bantu Divergence – Convergence Theory*. Dar es Salaam: Dar es Slaam University Press.
- Massamba, D. P. B., Y. M. Kihore & Hokororo, J. I. (2004). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA); Sekondari na Vyu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mdee, J. S. (1998), *Sarufi ya Kiswahili: Sekondari na Vyu*, Dar es Salaam: Dar es Slaam University Press.
- Mlacha, S. A. K. (1995). "Fasihi Simulizi na Usuli wa Historia ya Pemba". Katika *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Mlacha, S. A. K, na Hurskainen, A (wah.). TUKI: Dar es Slaam University Press.
- Nunan, D. (1992), *Research Methodology in Language Learning*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Nurse, D. & Hinnebusch, T. J. (1993). *Swahili and Sabaki*. California: California University Press.

- Nurse, D. & Spear, T. (1985). *The Kiswahili: Reconstructing the History and Language of an African Society*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.
- Polomé, E. C. (1967). *Swahili Language Handbook*, Washington D.C: Center for Applied Linguistics.
- Prasad, T. (2012). *Acouse in Linguistics*. New Delhi: PHI Learning Private Limited.
- Stigand, C. H. (1915). *Dialect in Swahili*. London: Cambridge University Press.
- Sture, J. (2010). *Ethics in Research Project*. Some Guidance on Recognising and Addressing Ethical Issues, Bradford: University of Bradford Press.
- Temu, C. W. (1980). *Lahaja za Kiswahili*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Toleo la 2)* Nairobi: Oxford University Press.
- Whiteley, W. (1956). *Kimtang'ata: A Dialect of the Mrima Coast*. Kampala: East African Swahili Committee.
- Whiteley, W. H. (1958). *The Dialect and Verse of Pemba*. Kampala: East African Swahili Committee.
- Yule, G. (1985). *The Study of Language*. London: Cambridge University Press.

**VIAMBATISHO****Kiambatisho A: Dodoso****CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA  
KITIVO CHA FANI NA SAYANSI ZA JAMII  
IDARA YA ISIMU NA TAALIMU ZA KIFASIHI****MWONGOZO WA MASWALI YA UTAFITI****(DODOSO)**

Utafiti kuhusu Tofauti za kifonolojia na kimofolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini

1. Naomba unieleze wakazi wengi wa eneo hili asili yao ni wapi?
2. Kuna tofauti zipi za kifonolojia baina ya watu Kaskazini na Kusini Pemba.
3. Kuna tofauti gani za kimofolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini?
4. Nitajie maumbo ya nomino na vitenzi unayoyajua?
5. Unadhani kwa kiasi gani watu wa kaskazini wanatofautiana na kusini katika usemaji?
6. Ngeli za nomino za Kipemba cha Kaskazini na cha Kusini zina tofauti na za maeneo mengine?

*Ahsante kwa msaada wako*



**Kiambatisho B: Hojaji**

CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA  
KITIVO CHA FANI NA SAYANSI ZA JAMII  
IDARA YA ISIMU NA TAALIMU ZA KIFASIHI

**HOJAJI YA KUCHUNGUZA TOFAUTI ZA KIFONOLOJIA NA  
KIMOFOLOJIA**

**Maelezo:**

- Baadhi ya maneno ya Kiswahili hutamkwa tofauti baina ya maeneo Kaskazini na Kusini.
- Tafadhali wasikilize kwa makini watumiaji wa Kiswahili wa eneo unaloishi na uandike matamshi ya maneno kulingana na zinavyotamkwa katika eneo lako.

<b>Kiswahili Sanifu</b>	<b>Kipemba cha eneo lako</b>
1. mke	
2. mkia	
3. mkono	
4. mlima	
5. msitu	
6. shavu	
7. chota	
8. choto	
9. chaza	
10. chawa	
11. chungwa	
12. chumvi	
13. chuchuka	
14. tapishi	
15. moshi	
16. tapishi	
17. ombi	
18. moshi	
19. serikali	
20. shingo	
21. mpishi	

<b>Kiswahili Sanifu</b>	<b>Kipemba cha eneo lako</b>
22. matusi	
23. sikio	
24. sindano	
25. sanjari	
26. joma	
27. jani	
28. dema	
29. kidevu	
30. diko	
31. lindi	
32. lenga	
33. birika	
34. urimbo	
35. mwereka	
36. kibatari	
37. boje	
38. uzia	
39. pumua	
40. vukuto	

**Kiambatisho C: Matini Mbalimbali Zilizorekodiwa**

**Matini na.1: Mazungumzo ya Bibi na Mtafiti (*Kutoka Kusini*)**

- Bibi: Basi mmakuona kulya upokuwa ukaja.
- Mtafiti: Ha umenijuaje bibi?
- Mwajuma: Ama! Amba n'geni hanyagili ntapomwona ntantambuya.
- Mtafiti: Ha! Bibi hanyagili ndiyo maanaye n nini?
- Mwajuma: Ndo ivyo hanipoteyi.
- Mtafiti: Mwalimu Machano hasomeshi tena Mwambe?
- Mwajuma: Enhe! Kende Darisalama kuzinga maisha... ela nsikiavyo webiwa na sasa washarudi... yule pale katoko uso ja miye angoja tuchezee jembe shirika. Ve katazinyorosa wa?

**Matini na. 2: Mazungumzo ya Jamaa Wawili (*Kutoka Kaskazini*)**

- Jamaa1: Ha aloo kunfanya vi: leyo?
- Jamaa 2: Ha amba nami nanza kuja.
- Jamaa1: Ha kunkujafiswa ni ani tena? Nauku kunambili kukwiji ta uku!
- Jamaa 2: Ha ntu kwawo aga? Natotoma vivyo ivyo ta nawona watu wannelekeza
- Jamaa 1: Ile ng'ombe yalya majani vyo.
- Jamaa 2: He! Ebu nambiya kwani itendeje?
- Jamaa1: Ilyi majani ya mpangapanga... tokyo jana haimwagaa.
- Jamaa 2: Mwanangu kwako ajaakizinga ni?
- Jamaa 1: Aja akicheza na wenziwe.
- Jamaa 2: Jana kambili kuu jongwe.

Jamaa 1 : Selipata ... amba lingili vong'oni.

Jamaa 2 : Basi hapekalika tena apo.

**Matini na.3 : Wakati wa Uchaguzi (*Kutoka Kaskazini*)**

“... kula ukikurubiya uchaguzi basi miye natunguka. Kwa sبابu nshi ii haina domokirasiya ta kidinya. Kula siku utasikiya ridiyo zatangaaza kuwa mfumo wa vyama vingi wanrhusu kula ntu kujiunga na kyama atakayo na kuchaguwa mgombeya atakaye. ... ela kumbi watu wa sirikali n waongo. Mwaka tisiini na tano miye nelala vituwani nyezi sita. Kisa na sبابu nekuwa wakyala wa Kafu... mwinzangu e Babe Shume... efanya goya ta akitiwa kuchani m mapolisi... ama siku eliyogwiwa etuugwa taaa haluwa ikawa ngumu. Siku zote nkaidi hafaidi... ati tushaambiwa kuwa twazingwa m mapolisi, akijitiya kujyamini ati mwinzetu m bulugadi. Basi ekwendeswa jela mwishowe enyolewa pare. ...Miye siyasa za Zanziba nazijuwa uzuuri... bankuu Mfaki, vyama vingi kuwanza tu enita akiniusiya. Enambiya mambo matatu. Ntu akiwa kiongozi katika kyama kya upinzani mambo matatu lazima moja awu maili awu pya yosi yaenza mpata maana awakera watawala. Kwanza, kama ni mfanyakazi wa sirikali... watankwama. Pili, atafisidiwa n wenziwe na tatu, aezapigwa bunduki. ...miye sifanyi ubishi na ntu nsiyemmudi sichezi na dola ta siku unusu...

**Matini na.4: Mazungumzo ya Babu na Mgeni (*Kutoka Kaskazini*)**

Mgeni : Babu shikamoo.

Babu : Marahaba mgeni wa usiku hukaribishwa kitanda ...

Mgeni : Aka Babu!

- Babu : Enhe, siye kama apa tena hatuna lyolyote maji yakitoka yanatoka.
- Mgeni : Kwani babu uliwahi oa?
- Babu : Enhe! Tena kapata wana tisiaa ela sabaa werudi wakabakiya wawili. Wa kwanza etwa Kihogo.
- Mgeni : Hulisikiya ilyo jina likatajwa mamaangu alinihadisiya.
- Babu : Mameyo yu?
- Mgeni : Asha Ali Hamadi uyu wa Mkoa.
- Babu : Basi weye mwana yangu ati.
- Mgeni : Babu basi tutajaonana siku nyengine Mungu akitujaaliya.
- Babu : Haya karibu tena.

**Matini na. 5: Mazungumzo ya Kijakazi na Siti (*Kutoka Kusini*)**

- Kijakazi: Dade mmamwona shemegi njiyani kanababaika ovyo.
- Siti: Hana kazi kanasemaje?
- Kijakazi: Shemegi dadiyo nshamwacha ela mmakutwa nkiliyo naona takuwa na marazi. Kuna marazi mana hujitambuwa apoupomwacha? Ama bwana yule kana matatizo gani kaono ja ivi?
- Siti: Mamiye hataki mazumuni yao kufa kwa Kombo nisipate muume ela kwa vile Muungu kaniumbu na riziki sikoso.
- Kijakazi: Mwenyezi Mungu ve haharibu hutengeza tu lina heri ilyo lishapita kunaja kubwa zaidi pito ya ilyo. Katakuja kurejeya ela kama kutakubali rejewa taona wacheza watu shere.

Siti: Hende hasubutu nasikiya Machano kanrapu kamwambili kunatuhanisi kikwelikweli shehe nzima, mwalimu nzima kunaswalisha kunaichezeya talaka umakusudiya ndugu yangu umuuwe lakini kutajuwa mwinyiwo.

Kijakazi: Sitahamili dade yangu lakini riziki ikaja ukaona kunacheka nayo rohoni usiitowe ndo kutakapopata maliwaza ukajapusa sahou.

Siti: Basi na uyo nkewe mwengine kanangoja avyae tu kanyambili katamwacha.

Kijakazi: Abaki ujane! Kwani?

Siti: Siji mwinyiwe lilomo ndani ya nafusi yakwe katajiju mana kanyambili miye mbaa ela naye zuri etiwa piko n Muungu isoyawa kutajasikiya.

Kijakazi: Kanipe karafuu kidogo.

Siti: Kwani shemegi kasharudi?

Kijakazi: Bado siji naye kuwa hashaowa uko naona hazuku.

Siti: Siji e watu waume kunazani watu? Ndo mana Mungu akawapa kiya basi karafuu izo za ni? Akaja tajakupa.

Kijakazi : Kutavitambuwa vipi nawe huna simu? Kanipe ntaka ja vile mpyampya.

Siti: Sikupa hadi arudi, mume hakongo kutankongesha kwa tabiya zako. Nendavyo uko usiku wangiya.

Kijakazi: Kweli kwa heri akaja kutaniona japo mara moja.

### **Matini na.6: Mazungungumzo ya Bibi na Mtafiti (*Kutoka Kusini*)**

Bibi: Karibu n'geni yetu nkutendele chai.

Mtafiti: Chai basi tu... bibi asante.

Bibi: Ntu kwenda pahala kutembeya asile kyokyote huwa vipi ntu weye utakavyokwenda tongowa ntu weye uko kwenu?

Bibi: Mie sinwi chai mana ilyo tumbo lyangu si zuri nasema lada ndiyo safari.

Mtafiti: Ya wapi bibi?

Bibi: Aka! Si kuno kwetu uko ahera ndo kwetu kuno matembezi tu.

Mtafiti: Bi miaka mia watembea tu?

Bibi :Mjukuu yangu nyaka mia keli ipiti taanikiwa juwa ja ntu mmoja ekenikiwa juwa akaikiwa na paka na vitu vyakwe, paka kanaliya miye humwambiya bibi mbona hunakulya uyo paka kanakwambiya ulye ilikuwa Kengeja huko.

Mtafiti: Bibi kwa heri...

Bibi: Mjukuu yangu karibuni wendavyo na njaayo.

### **Matini na.7: Mazungumzo ya Bibi na Wajukuu (*Kutoka Kaskazini*)**

Mjukuu 1 :Bibi nasikiya zamani muume ekisuguliwa ati kweli?

Bibi : Apo kale sasa hayako tena ... muume akisuguigwa na shemegize mana si maumbuze... akisuguigwa kwa karafuu zikihushiwa uzuri... zinanuka to. Harusi akinafuzwa kunsuguwa muume anza apa nlaze ivi kula kitu akinafuzwa, ela sasa hayako tunaageya urembo.

Mjukuu 2 : Ntu muume akiikwa wa?

Bibi : Kichwa kikiikwa mapajani

Mjukuu 2 : Ha! Nawe kunampakata nkewo kama yeye?

Bibi : Muume akitaka hakatazwa ela nke hasa akitakiwa anfanzi muumewe maana hubembelezwa usiyone kama leyo hamuna mutambuwalyo ata mukifuzwa hamufuziki.

Tena hapo nyosi muvaa kanga... upande wakwe upande wako, ukianza usoni kunsuguwa kwa liwa na uko kwa bankuu. Sehemu zilizobaki ukintiya karafuu kumuavya nongo na kuavya mavune, karafuu hatiwa usoni itamuwasha.

Mjukuu 1 : Bi hamukitahayari? Kutenda kama ivo hasa kwa bi harusi kuntendeya muumewe ta hajazoweya ntu muume.

Bibi : Kutahayarini? Rabuda uwe humwebu, kulikuwa na Mwakombo Shaame akimwebu vyema muumewe hemuonjesapo shariya ekuwa akampeteya futi.

Mjukuu 2 : Ati zamani bi wanawali wangi hewekikutwa wari? Mana sasa wamajaa tele matomo. e kale ndo heweeko au tumasemwa tu watoto wa leyo?

Bibi : Kale heyako nadira ela sasa wari wote washakatwa tata. Maana juzi nekaa apo wakaja wanawali watatu wa Sebudawa wakasema kawasikiya e ntu nke ukitongozwa nenda we Siku ya kwanza utaona kama kuntafunwa ni mbu apo tena utazoweya.

Mjukuu 1: Bi tupo tuliokutwa wari ela nyiye watu wa zamani mutasikiya wanawali wa leyo n watukutu hawatulili na zamani nawo nasikiya wekuwa ivyo ivyo wengine.